SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 4

**RIPOTI MAALUM -2**
**Risasi iliyomuua mwanakijiji mgodini inavyozua mtafaruku**




UKURASA 9

Jumapili Aprili 10, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0580911
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Samia: Kazi kubwa ni kurejesha umoja

**ASISITIZA** ndiyo njia pekee kumuenzi Nyerere, asema watu walikengeuka wakaanza kujuana kwa ukabila, udini na ukanda...*Endelea ukurasa 2*



Rais Samia Suluhu Hassan, akionyesha vitabu vitatu vya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, baada ya kuvizindua katika mdahalo wa kumbukizi ya miaka 100 ya kuzaliwa kwake, katika viwanja vya Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere, Kibaha, Pwani jana. **Picha ndogo:** Rais Samia, akimkabidhi tuzo Makongoro Nyerere, ambaye ni mtoto wa Mwalimu Nyerere kwa niaba ya familia. **PICHA: IKULU**

## Mbunge asema kuna mchezo mchafu bidhaa kupanda bei

UKURASA 2

## Faini 200,000/- kuvuta sigara hadharani au jela miezi sita

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA, POLISI KAZI IPO LEO UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6



Msafara wa waendesha baiskeli kitaifa ulioanzia safari yao, mkoani Dar es Salaam, Aprili 7 mwaka huu, ukipita jijini Dodoma juzi, kuelekea Butiama, mkoani Mara, ambapo safari yao inatarajiwa kutumia siku tano hadi kufika, kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 100 ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge: Kuna mchezo mchafu bidhaa kupanda

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Kyerwa, Innocent Bilakwate (CCM), amesema kupanda kwa bei ya bidhaa hakutokani na kupanda kwa bei ya mafuta, bali kuachiwa kwa wafanyabiashara kujitawala na kujiamulia wanavyotaka.

Alitoa kauli hiyo bungeni jijini hapa juzi jioni alipochangia majadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Bilakwate alisema takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) za Desemba mwaka jana zinaonyesha kuwa bei ya mafuta katika Jiji la Dar es Salaam zilikuwa Sh. 2,510 na kwa Kigoma katika Wilaya ya Uvinza zilikuwa Sh. 2,754 kwa lita.

Alisema kuwa kwa mwezi Februari mwaka huu, bei ya mafuta ilishuka ikawa Sh. 2,480 Dar es Salaam na Sh. 2,720 kwa Uvinza mkoani Kigoma, hivyo bei ilipungua kwa Sh. 30.

Mbunge huyo alisema kuwa Machi mwaka huu, bei ya mafuta Dar es Salaam ilikuwa Sh. 2,500 na Sh. 2,784 kwa Uvinza mkoani Kigoma.

"Waheshimiwa wabunge, lazima tueleze ukweli, bidhaa zilizopanda hazitokani na upandaji wa mafuta. Ukiangalia bei za EWURA, haiwezekani Sh. 60 iliyopanda ndiyo iongeze bei kiasi hiki," alifafanua.

Bilakwate alisema jimboni kwake kuna aina mbili za sabuni wanazozitumia ambapo Januari mwaka huu, aina ya kwanza ilikuwa inauzwa Sh. 1,000, lakini sasa zinauzwa Sh. 3,500 wakati aina ya pili ilikuwa inauzwa Sh. 2,000, sasa imepanda hadi Sh. 5,000.

"Hivi hii Sh. 60 iliyoongezeka katika mafuta ndiyo imependisha bei ya bidhaa kiasi hiki? Kwenye mafuta ya kula yaliyokuwa yakiuzwa Sh. 1,700, sasa yanauzwa Sh. 3,500, hii haikubaliki!" alilalamika.

Mbunge huyo alisema kuwa kwenye vifaa vya ujenzi nako hali ni mbaya, akifafanua kuwa mwaka jana, aliagiza vifaa vya ujenzi kwa gharama za Sh. milioni 18, lakini aliporejea kwa mwagizaji juzi kutaka vifaa hivyo hivyo, aliambiwa bei yake kwa sasa ni Sh. milioni 35.

Alisema suala la kusema makali hayo yanatokana na kupanda kwa mafuta yazungumzwe kuanzia Aprili 6, mwaka huu, siyo miezi mitatu iliyopita.

"Miezi mitatu iliyopita bei ya mafuta haikuwa imependa kiasi cha kupandisha namna hii bei ya bidhaa. Kitu nilichofuatilia, kupanda kwa bei kunasababishwa na hawa watu, wameachiwa kujitawala, kufanya wanavyotaka.

"Mimi ninaomba tumsaidie Mheshimiwa Rais, tusiende na hoja kuwa bidhaa zimepanda kwa sababu ya mafuta," mbunge huyo alitoa angalizo kwa wenzake.

**SHABIBY BEI YA MAFUTA**

Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby (CCM), amesema serikali ikiruhusu uagizaji huria wa mafuta kufanyika sambamba na uagizaji wa pamoja, bei ya nishati hiyo itashuka hadi Sh. 1,800 kwa lita.

Akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari juzi jioni kwenye viwanja vya Bunge kuhusu ushauri wake alioutoa bungeni Jumatano wa serikali kuruhusu uagizaji huria wa mafuta katika kipindi hiki ambacho nishati hiyo imependa kutokana na vita kati ya Russia na Ukraine, Shabiby alisema:

"Tukisharuhusu wafanyabiashara mmoja mmoja kuagiza mafuta, bei ya mafuta nchini itashuka sana, yatafika hadi Sh. 1,800 kwa lita. Wafanyabiashara wanajua mahali pa kuyapata mafuta kwa bei nzuri na kuyauza kwa bei rahisi.

"Huu utaratibu wa kuagiza mafuta kwa pamoja unaondoa ushindani wa kibiashara kwenye mafuta. Serikali iruhusu wanaoagiza kwa pamoja waagize na wanaoagiza mmoja mmoja walete, yenyewe ibaki kudhibiti bei kikomo, kukusanya kodi na kuangalia ubora wa mafuta.

"Watasema ninasema hivyo kwa sababu nina vituo vya mafuta, jamani mimi nina vituo viwili tu - kimoja hapa Dodoma na kingine jimboni Gairo. Kuna watu wana maslahi yao katika hili, hata baadhi ya vyombo vya habari vinatumika, lakini anayeumia ni mwananchi wa kawaida kutokana na mafuta kuuzwa kwa bei kubwa."

**MCHANGO BUNGENI**

Katika mchango wake bungeni Jumatano, Shabiby alisema kuna haja serikali kuruhusu wafanyabiashara mmoja mmoja kuagiza mafuta nje ya nchi, akiamini ndiyo njia sahihi ya kukabiliana na kupaa kwa bei ya nishati hiyo nchini.

Alisema kwamba utaratibu wa sasa wa kuagiza mafuta kwa pamoja ni tatizo kwa kuwa hautoi nafasi ya ushindani wa biashara miongoni mwa wafanyabiashara wa mafuta.

"Wanasema 'ukiruhusu wafanyabiashara mmoja mmoja aagize mafuta, watakwepa ushuru', jamani meli zote zinashusha kwenye mita, hamuwaamini TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania)? Ile mita imekufa mara ngapi? Imekufa mara nyingi zaidi kipindi hiki kuliko zamani.

"Serikali haiwezi kutoa kodi kwenye mafuta, ikitoa kodi kwenye mafuta, nchi hii haina dawa, haina mishahara, hatuwezi kutoa kodi, lazima kodi iwapo kwenye mafuta.

"Watanzania wa sasa wana akili, kukiwa na wizi wanajua kwamba hapa kuna tatizo, kama kuna 'dili' wanajua hapa hili ni 'dili'. Nilionya mapema hapa bungeni kwamba ununuzi wa mafuta kwa pamoja utaleta shida, sasa imekuwa ni moto. "Nimeshasema na ninarudia kusema, ilikuja kampuni moja hapa ya India, ikashusha bei ya mafuta kwa kiwango kikubwa lakini ikapigwa vita, ikazuiwa mtu binafsi kuleta mafuta.

"Matokeo yake ni kwamba ukishanunua mafuta kwa pamoja, wote mnakuwa na bei moja, nani atashusha? Hakuna tena ushindani kwenye mafuta, yule jamaa wa India ikabidi auze kampuni yake kwa watu waliopo hapa.

"Kuna kampuni zinauza mafuta kwa robo ya bei ya dunia. Ukimruhusu mfanyabiashara alete mafuta, atayapata ya bei rahisi, nchi hii inatumia lita milioni 400 kwa mwezi, lakini ukishasema tu hapa, utasikia wanasema 'huyu Shabiby atakuwa mwizi wa mafuta huyu' wakati wezi mko huko huko, ndiyo majambazi," alisema.

# Samia: Kazi kubwa ni kurejesha umoja

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema kuna kazi ya kuirudisha nchi katika umoja baada ya kutetereka kutokana na watu kujuana kwa udini, kabila, ukanda na itikadi.

Amesema Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alilijenga taifa lenye umoja na mshikamano na alipinga ubaguzi wote wa udini, ukanda na ukabila, hivyo ni wajibu wa Watanzania kupinga vitu hivyo ikiwa ni sehemu ya kumuenzi.

Samia aliyasema hayo jana kwenye mdahalo wa kitaifa wa kuadhimisha miaka 100 ya kuzaliwa kwa Mwalimu Nyerere, uliofanyika katika Shule ya Uongozi, Kibaha mkoani Pwani.

"Mwalimu alijenga taifa lenye umoja na mshikamano kwa kupinga ubaguzi wote wa udini, ukanda, ukabila na itikadi.

"Na hapa kuna kazi ya kufanya kidogo na panaumiza kichwa kidogo. Naomba nirejee alichosema Abubakari Liyongo kwamba hapo katikati tulitetereka kidogo, tukaanza kujuana kwa rangi, udini, ukabila na ukanda, lakini pia kwa itikadi, hivyo tuna kazi ya kurudi kuifanya Tanzania kuwa moja," alisema.

"Ni muhimu Watanzania tuwe kitu kimoja. Hilo ndilo Hayati Mwalimu Nyerere alilifanya, alihimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kabla na baada ya uhuru kama nyenzo ya kujenga umoja wa kitaifa," aliongeza.

Rais Samia alisema Hayati Nyerere amewaachia somo kubwa Watanzania la kuwa wazalendo kwa taifa kwa kuwa alilipenda na kujitoa mhanga kwa ajili ya Watanzania.

"Somo kubwa alilotufundisha Hayati Mwalimu Nyerere ni uzalendo kwa taifa letu. Yeye (Nyerere) mwenyewe alikuwa mzalendo wa kweli, alilipenda taifa na alikuwa tayari kujitoa mhanga kwa ajili ya Watanzania.

"Uzalendo wake ulijionyesha wakati wa kupigania uhuru alipoacha kazi ya ualimu na kujikita katika kulikomboa taifa na wenzake na akapitia magumu na changamoto nyingi kwa ajili ya kulikomboa taifa hili," alisema.

Pia alisema Mwalimu Nyerere aliiwezesha lugha ya Kiswahili kukubalika na Waafrika na sasa ni lugha rasmi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Utamaduni (UNESCO) kuitengea siku yake maalumu.

Rais aliagiza Chuo cha Taifa cha Siasa, Uongozi na Maadili cha Mwalimu Nyerere kilichoko Kibaha, kuwa kituo cha kuhifadhi kumbukumbu za historia za waasisi ambazo zitatumika kufundisha, kuongoza nchi kwenye mambo mbalimbali. Alisema kwa kufanya hivyo itakuwa njia ya kumuenzi Mwalimu Nyerere.

**MAKONGORO ANENA**

Mtoto wa Nyerere, Makongoro, alieleza namna baba yake alivyomshirikisha nia ya kutaka kung'atuka mwaka 1980 na wasiwasi aliokuwa nao.

Makongoro ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Manyara, alisema kabla ya kung'atuka, Mwalimu Nyerere alimshirikisha nia ya kufanya hivyo na akaelewa hoja zake zilizokuwa na mashiko.

Alisema jambo ambalo alimpinga wakati akimshirikisha ni kwamba ataishije bila kuwa mtoto wa Rais.

"Hoja zote nilimwelewa Mwalimu Nyerere, lakini wasiwasi wangu ilikuwa nimeshazoea kuishi kama mtoto wa Rais. Sasa itakuwaje akiondoka? Ina maana nitaishi kama mtoto wa Mwalimu na siyo Rais," alisema.

"Pamoja na yote yaliyotokea ya Mwalimu kung'atuka na baadaye kufariki dunia, nashukuru mpaka sasa ninaishi kama mtoto wa Mwalimu, nimekuwa nikifanya mambo mengi kwa ajili ya jina lake na hata leo nipo hapa kwa ajili yake yeye.

"Ukitafuta mambo ambayo Makongoro amewahi kufanya katika nchi hii, unaweza ukatafuta mpaka ukome, lakini nipo kwa ajili ya Mwalimu. Ni kupitia jina lake, nimesafiri nchi mbalimbali, zikiwamo Afrika Kusini na Namibia kuchukua tuzo ya Mwalimu Nyerere, maeneo ambayo nilikuwa sijawahi kufika," aliongeza.

Makongoro alisema Mwalimu Nyerere alipenda sana suala la ubinadamu na alikuwa na maono ya mbali ambayo baadhi aliyaona na mengine hakufanikiwa kuyaona ikiwamo ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme, pamoja na serikali kuhamia Dodoma.

Naye Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, alisema vitabu vya maandiko ya Mwalimu Nyerere vilivyozinduliwa na Rais Samia, vitasaidia katika kufanya marejeo kwenye vyuo vikuu kikiwamo Chuo cha Uongozi.

Mwanazuoni Profesa Issa Shivji, ambaye ni moja ya waandishi wa kitabu cha Historia ya Mwalimu Nyerere alisema wasifu zote za Hayati Mwalimu Nyerere zilizowahi kuandikwa miaka iliyopita ziliandikwa na waandishi kutoka nchi za nje, lakini kwa mara ya kwanza wasifu huu wa sasa umeandikwa na waandishi wa Tanzania.

HABARI KITAIFA

## Mvua yazua maafa wananchi kata mbili

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

MVUA kubwa iliyonyesha kuanzia majira ya saa 7:00 usiku hadi saa 2:00 asubuhi katika maeneo mbalimbali ya Songea mkoani Ruvuma, imesababisha daraja la Mto Mwembe Chai, linalounganisha kata za Matarawe na Mjimwema kubomoka.

Hatua hiyo imesababisha kukatika kwa mawasiliano baina ya maeneo hayo na kufanya magari, pikipiki na watembea kwa miguu kushindwa kupita.

Kwa muda sasa, mvua zinaendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali ya mkoa na kusababisha kuwapo kwa ubovu wa miundombinu ya barabara ikiwamo ile ya kutoka Majengo kwenda Ruvuma, Liwena hadi Mpitimbi.

NIPASHE ilifika kwenye eneo la tukio ambako daraja limebomoka na kukuta umati mkubwa wa watu waliofika kushuhudia akiwamo Diwani wa Mjimwema, Sylvester Mhagama.

Akizungumza katika eneo hilo, Mhagama alisema kubomoka kwa daraja hilo ni tatizo kubwa kwa wakazi wa Manispaa ya Songea kwa kuwa barabara ya kutoka Zimamoto hadi Mjimwema inatumiwa na wananchi kwenda kupata matibabu katika kituo cha Afya cha Mjimwema.

Pia alisema wafanyabiashara wanaoishi katika maeneo ya Ruwawasi na Mjimwema wanapotaka kwenda kupata mahitaji Songea mjini ambako kuna soko kuu na Soko la Manzese, wanashindwa kupita, hivyo kulazimika kupita barabara ya kuzunguka kitambo kirefu kutoka Msamala, Bombambili, Ruhuwiko hadi mjini.

Mhagama aliiomba serikali ione umuhimu wa kuchukua hatua za haraka za kulifanyia matengenezo daraja hilo ambalo ni kiungo kikubwa cha barabara kutoka Songea mjini kwenda Mjimwema ili wananchi waondokane na kero inayowakabili.

Diwani huyo alisema sasa ni mara ya tatu kuvunjika kwa daraja la Mjimwema kwa kuwa mwaka jana wakati wa mvua, lilibomoka na kujengwa Februari ,mwaka huu.

Naye Diwani wa Ruvuma, Issa Telela, alionyesha kusikitishwa kwake baada ya miundombinu ya barabara katika kata hiyo ya kutoka Majengo kwenda Ruvuma, Liwena hadi Mpitimbi pamoja na barabara ya kutoka Ruvuma kwenda Kipera zimekithiri kwa kuwa na mashimo makubwa.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Wahabu Nyamzungu, alisema hatua za haraka zimechukuliwa kwa kuhakikisha linatengenezwa na kuanza kutumika mara moja.

# Mbunge amshauri Rais Samia aimulike wakala uagizaji mafuta

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MBUNGE wa Sengerema, Hamis Tabasamu (CCM), amesema kuna haja Rais Samia Suluhu Hassan kuuangalia Wakala wa Ununuzi wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa haraka kwa sababu unaonekana utasababisha tatizo kubwa mbeleni.

Vilevile, amesema Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) linalidai Shirika la Umeme (TANESCO) Sh. bilioni 502, hivyo kuna haja serikali kuja na mpango bungeni wa kuonyesha namna itakavyolipa.

Alitoa angalizo hilo bungeni jijini hapa juzi jioni alipochangia majadala wa makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Mbunge huyo alisema TPDC ilipata fursa ya kuagiza mafuta kwa dola za Marekani milioni 26 hadi kufika nchini lakini maombi ya kupata kibali cha kuagiza yalikataliwa.

"Uzalendo hakuna kuko PBPA, Rais tunamwomba aiangalie PBPA kwa haraka mno, hawa watu watakuja kumletea tatizo kubwa kwenye nchi hii, hatuwezi kukubali," alitahadharisha.

Alisema kuwa Machi 22, mwaka huu, iliingia meli ya mafuta nchini yenye tani 39 lakini Shirika la Viwango (TBS) lilipoyapima mafuta, kulibainika asilimia 90 ya mafuta yalikuwa vizuri na asilimia 10 hayakuwa vizuri.

Mbunge huyo alisema meli hiyo iliondoka na kwenda kushusha shehena hiyo Bandari ya Beira, jambo ambalo alisema limesababisha serikali kupoteza Sh. bilioni 14 wakati kulikuwa na uwezekano wa kushusha mafuta mazuri na kuyaacha yasiyokidhi viwango.



Mafundi wa Taasisi ya Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), wakionyesha kwa waandishi wa habari za utafiti na ubunifu, stendi ya kutundikia dripu walizozitengeneza, walipofanya ziara katika taasisi hiyo, eneo la Njiro, jijini Arusha mapema wiki hii, baada ya kupata mafunzo ya sayansi na teknolojia yalioandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Moja ya miradi inayofanywa na TEMDO ni utengenezaji wa vifaa tiba kwa ajili ya kutumika hospitali. **PICHA: WOIMDE SHIZZA**

# Faini 200,000/- au jela kuvuta sigara hadharani

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imesema ni kosa kisheria kuvuta sigara hadharani au kwenye maeneo ya mikusanyiko na atakayebainika kufanya hivyo atatozwa faini ya Sh. 200,000 au kutumikia adhabu ya kifungo cha miezi sita jela.

Meneja wa Kanda ya Mashariki wa TMDA, Gloria Matemu, aliyasema hayo jana katika Soko Kuu la Kariakoo, wakati wa kampeni ya kutoa elimu katika maeneo ya mikusanyo kuhusu madhara ya kutumia tumbaku na adhabu zake.

Alisema TMDA imepewa jukumu la kudhibiti matumizi ya tumbaku kwa lengo la kutoa elimu kuhusu matakwa ya sheria namba 121 kuanzia Aprili 30, mwaka jana.

"Ukibainika unavuta tumbaku hadharani au katika mikusanyiko utatozwa faini ya Sh. 200,000 au kutumikia adhabu ya miezi sita jela," alisema.

Hivyo, aliwataka wamiliki wa kumbi za starehe na masoko kutenga maeneo maalum ya kuvutia sigara kwa sababu watu wengi wanaathirika kutokana na watu wachache wanaovuta sigara.

Matemu alisema TMDA imefanya kampeni ya siku tano ya kutembelea kwenye maeneo yenye mikusanyiko mikubwa ya watu kama vituo vya mabasi na masoko, ili kuwaelimisha kuhusu madhara na namna sheria inavyofanya kazi.

Alisema kampeni hiyo imesaidia kufikisha elimu kwa wakazi wa Manispaa ya Ilala na lengo kuu ni kuwafikia Watanzania wote wafahamu kuhusu jukumu hilo la TMDA katika kudhibiti matumizi ya tumbaku ili kupunguza madhara yatokanayo na uvutaji huo.

Mkaguzi wa TMDA, Kanda ya Mashariki, Jafari Tolo, alisema takwa la sheria ni kuzuia uvutaji wa sigara kwenye mikusanyiko ya watu na wamiliki wa maeneo yanayokusanya watu kutenga maeneo maalum ya wanaovuta kuvuta bila kuathiri wasiovuta.

Alisema pia maeneo yenye mikusanyiko kunapaswa kufungwa vifaa vya kubaini endapo kuna mtu anavuta sigara katika maeneo yasiyoruhusiwa.

Ofisa Afya wa Soko la Kisutu, Aron Matei aliishukuru TMDA kwa elimu waliyotoa na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari kuhusu uvutaji wa sigara katika maeneo yasiyo rasmi.

RIPOTI MAALUM -2

# Risasi iliyomuua mwanakijiji mgodini inavyozua mtafaruku

**Na Mwandishi Wetu, KISHAPU**

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii wiki iliyopita ilibeba simulizi ya kina itokanayo na ushuhuda wenye ufafanuzi kilichojiri kuhusu mauaji ya kijana mwanakijiji Cosmas Hamis (23), aliyekuwa anaishi jirani na mgodi wa almasi wa El Hilali wilayani Kishapu mkoani Shinyanga. Je, nini kinafuata? Endelea kufuatilia undani wa suala hilo, ikiwamo ngazi ya kitaifa:**

----------------------------------------------



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, George Kyando.

**KUTOKA POLISI**

Nipashe inatua kwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi George Kyando, kujua mustakabali wa vitendo hivyo vya mauaji dhidi ya raia migodini.

Kamanda Kyando anakiri kuwapo kwa tukio la mauaji dhidi ya kijana Cosmas lakini anasita kulizungumzia kwa kina kwa maelezo kwamba liko kwenye uchunguzi wa vyombo vya dola.

"Ni kweli tukio hilo lipo lakini siwezi kulizungumzia zaidi kwa sababu bado liko kwenye uchunguzi," alisema Kamanda Kyando, alipowasiliana na Nipashe Ijumaa Machi 25, mwaka huu majira ya saa 10 jioni.

Nipashe ilipotaka kujua sababu za Jeshi la Polisi Mkoa wa Shinyanga kutoa fedha kwa familia ya kijana Cosmas kwa ajili ya gharama za usafirishaji wa mwili wa marehemu, Kamanda Kyando alisema:

"Ile familia ina hali ngumu kiuchumi. Ililiomba Jeshi la Polisi litoe gari ili kusafirisha mwili kutoka hospitalini kwenda huko kijijini (Igumangobo). Sisi tuliwaambia hatuwezi kuwapa gari kwa sababu hatukuwa na mafuta ya kwenda huko kijijini kwao.

"Tuliuomba uongozi wa mgodi usaidie katika hilo. Mgodi ukatoa laki moja (Sh. 100,000) kwa ajili ya kusafirisha mwili. Kwa hiyo, hiyo laki moja haikutolewa na Jeshi la Polisi, bali ilitolewa na mgodi."

Alibainisha kuwa kumekuwa na vitendo vya wananchi kuingia ndani ya migodi ya almasi iliyoko eneo la Mwadui wilayani Kishapu wakiwa kwenye vikundi vya kati ya watu 200 na 300 kwa lengo la kuiba mchanga wa madini, lakini sasa vimepungua baada ya ulinzi kuimarishwa.

"Migodi iliyopo Mwadui ipo kisheria, hivyo wananchi kuendelea kuingia humo ni kosa, na ndiyo maana hata wakijeruhiwa na walinzi, huwa hawaji kutoa taarifa polisi kwa sababu wanajua watakamatwa na hivyo kwenda kujitibu wao wenyewe.

"Ninaomba mwandishi wa habari uandike kabisa kuwa 'Kamanda wa Jeshi la Polisi Shinyanga anaonya wananchi wasiendelee kuingia ndani ya mgodi kuiba mchanga wa madini, kwa sababu huo ni uhalifu na kuna walinzi wana silaha kali'," Kamanda Kyando alionya.

**KAULI YA DC**

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu na Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya hiyo, Joseph Mkude, anaungana na Kamanda Kyando kwamba kitendo cha wananchi kuingia ndani ya migodi iliyoko Mwadui na kuiba mchanga wa madini ni kosa kwa kuwa migodi hiyo ipo kisheria.

Kukabiliana na vitendo hivyo, Mkude anasema viongozi mbalimbali wilayani hapa wamekuwa wakitoa elimu kwa wananchi kupitia mikutano ya hadhara, wakiwahimiza kulinda uwekezaji lakini baadhi yao bado wanaendelea kuingia migodini kinyemela kwa lengo la kujitafutia kipato licha ya kutambua kwamba ni makosa kufanya hivyo.

"Migodi ya almasi iliyopo Mwadui ipo kisheria na ni makosa kuingia ndani ya migodi kinyume cha utaratibu. Niwaombe tu wananchi wafuate sheria za uwekezaji na kuacha kuingia kwenye migodi hiyo," Mkude anaagiza.

Hata hivyo, kutokana na kuwapo matukio ya wananchi kuendelea kuingia kwenye migodi hiyo kunakochangiwa na ugumu wa maisha, Mkuu wa Wilaya anasema wamezungumza na wawekezaji wa migodi kuangalia namna ya kuisaidia kiuchumi jamii inayoizunguka migodi yao ili wasiendelee kuivamia.

"Migodi iliyopo Mwadui inazungukwa na vijiji 11 na sasa tumeongeza kijiji kingine kipya na kufika vijiji 12. Tumeshazungumza na uongozi wa migodi kuona namna ya kuwasaidia wananchi kiuchumi kupitia miradi ya kilimo na ajira kwa vijana ndani ya mgodi ili wafanye shughuli ndogo ndogo," Mkude anasema.

**WATETEZI WA HAKI**

Wakili Joyce Komanya, Ofisa Mipango Mwandamizi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) anayeshughulika na haki, uwajibikaji na mazingira, katika taarifa yake rasmi kuhusu sakata hilo, anatamka:

"Serikali ina wajibu wa kuhakikisha inatoa ulinzi kwenye masuala ya haki za binadamu ikiwamo haki ya kuishi. Mgodi unaomilikiwa na El Hilali ni kati ya migodi inayoongoza kwa kipindi hiki kuwa na matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwamo mauaji yanayopoka haki ya kuishi.

"Unyanyasaji huo umekuwa ukiripotiwa sana na wakazi wa maeneo hayo na umekuwa ukifanywa na askari wanaolinda mgodi huo.

"Tanzania ni nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa (UN)na Umoja wa Afrika (AU) na imeridhia mikataba mbalimbali yenye lengo la kumlinda mwananchi wake dhidi ya ukiukwaji na uvunjifu wa haki za binadamu.

"Uwekezaji usiozingatia haki za binadamu hauna faida kwa jamii husika wala nchi kwani hutweza utu wa wananchi hao.

"Serikali ikiwa na wajibu namba moja chini ya mikataba ya kimataifa na Mwongozo wa Kimataifa wa Haki za Binadamu na Biashara wa Mwaka 2011, ina wajibu wa kulinda wananchi wake na kuhakikisha washukiwa wakuu wa ukiukwaji wa haki za binadamu wanachukuliwa hatua kwa kufikishwa kwenye vyombo husika na mamlaka za kisheria.

"Hivyo basi, haki itendeke kwa kijana Cosmas na familia yake isaidiwe kwa kuichukulia hatua madhubuti kampuni inayomiliki mgodi huo."

**KATIBA YA NCHI**

Kwa kurejea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inatamkwa katika Ibara ya 14 kuwa kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake kwa mujibu wa sheria.

Ibara ya 13(6)(e) ya Katiba hiyo pia inapiga marufuku mtu kuteswa, kuadhibiwa kinyama au kupewa adhabu zinazomtweza au kumdhalilisha.

**WAZIRI WA SHERIA AFAFANUA**

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia suala hilo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kuna mazingira askari polisi analazimika kutumia nguvu, lakini akawa na angalizo kwamba hilo lisiwe kigezo cha kukatisha uhai wa watuhumiwa wa uhalifu kwa kuwa jukumu la kwanza polisi ni kuzuia uhalifu kwa kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani.

Waziri huyo ambaye ni mbobevu kisheria akiwa na taaluma ya ngazi ya shahada ya uzamivu kwenye eneo hilo, alifafanua kwa kina, akisema:

"Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, askari polisi anaruhusiwa kutumia nguvu pale panapohitajika 'self defence' (kujihami) kama anayemshambulia yuko 'armed' (ana silaha). Na hili si kwa polisi tu, bali mtu yeyote anaruhusiwa kisheria kutumia nguvu ili kujihami.

"Tatizo ninaloliona kwa sasa jamii imepotoka sana, inakimbilia kumtetea mhalifu aliyepigwa na vyombo vya dola, haiangalii madhara kwa yule aliyevamiwa na hata hatari ya kuibiwa kwa mali zake.

"Nimeliona hili nilipokuwa Waziri wa Maliasili (na Utalii), wahalifu wanaingia hifadhini kufanya ujangili, jamii inataka askari wawakamate kienyeji, askari wetu watakufa!

"Sasa, kilichotokea mgodini (El Hilali), kinatokana na mazingira, lakini askari wasitumie mwanya huo wa kisheria kukatisha uhai wa watuhumiwa wa uhalifu maana jukumu la kwanza la askari polisi ni kuzuia uhalifu kwa kuwakamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani."

**USULI NA HISTORIA**

Inaporejewa historia ya uchimbaji madini Tanzania, uwapo wa almasi kwenye eneo la Mwadui uligunduliwa mwaka 1940 na raia wa Canada, Dk. John Williamson, mtaalamu wa jiolojia aliyekuwa amebobea katika masuala ya madini.

Madai ya kisheria dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na walinzi wa migodi hiyo yalifunguliwa katika Mahakama Kuu ya England na Wales Mei, 2020.

Shirika lisilo la kiserikali la RAID lilidai kuwa na ushahidi wa madhara yanayotokana na walinzi wenye mikataba na wamiliki wa migodi, kuwapiga risasi wenyeji katika eneo la migodi, ikijumuisha vifo vya watu 10 na wengine 50 kupata majeraha tangu mwaka 2009.



Hamis Kushilimwa na mke wake, Yunge Sheka, wakiwa na picha ya marehemu mtoto wao, Cosmas Hamis, mbele ya kaburi alilozikwa katika Kijiji cha Igumangobo, wilayani Kishapu hivi karibuni.
PICHA: MPIGAPICHA WETU

HABARI KITAIFA

# Jafo apiga 'stop' kampuni uhifadhi, usafirishaji salfa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ametoa siku saba kwa Kampuni ya African Inland Logistics kusitisha usafirishaji na utunzaji wa kemikali ya salfa.

Pia ameitaka kampuni hiyo kufanya marekebisho katika usafirishaji na uhifadhi wa kemikali hiyo pasipo kuhatarisha afya za wananchi wanaoishi karibu na kiwanda chao.

Waziri Jafo alitoa agizo hilo jana katika Kata ya Sandali wilayani Temeke alipofanya ziara ya ukaguzi katika ghala la kuhifadhia kemikali ya salfa kwenye kampuni hiyo.

"Natoa maelekezo kwa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kusimamisha shughuli zote za ghala hili mpaka watakapofanya marekebisho katika usafirishaji na uhifadhi wa kemikali hii ya salfa katika ghala hili ambalo liko katika makazi ya watu.

"Tunapenda uwekezaji nchini lakini uwekezaji ni lazima kutunza afya za wananchi. Wahakikishe wanaposafirisha kemikali hii hamna hata punje moja inayomwagika"

Aidha, Waziri Jafo aliiagiza kampuni hiyo kufanya ukaguzi wa mazingira mara moja kwa mujibu wa sheria ya mazingira inavyotaka.

"Nyie mnafanya kazi wakati hamna cheti cha aina yoyote, naagiza kufanya kaguzi ya mazingira, tunapenda uwekezaji uende mbele lakini siyo kudhuru wananchi kama hivi mnavyofanya" alisema Waziri Jafo.

Meneja wa NEMC Kanda ya Kusini Mashariki, Hamad Taimur, aliwataka wamiliki wa ghala hilo kutumia mifuko maalumu ya kufungashia kemikali ili kuepusha umwagaji hovyo barabarani wa kemikali hiyo wakati wa usafirishaji kutoka bandarini kwenda kwenye ghala hilo.

Diwani wa ya Sandali, Christopher Kabalika, alimshukuru Waziri Jafo kwa kutembelea eneo hilo na kujionea hali halisi iliyopo eneo hilo na kwamba umwagikaji huo wa kemikali ya salfa unaleta madhara kwa wananchi wa eneo hilo.

"Wananchi wako tayari kutoa ushirikiano kwa uwekezaji lakini kwa madhara ya namna hii hatutakua tayari kuvumilia," alisema Kabalika.

Wananchi wa eneo hilo walieleza malalamiko kwa Waziri Jafo kuhusiana na madhara wanayopata baada ya kemikali hiyo kumwagika katika bara-



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo (kulia), akitoa maelekezo kwa Meneja wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Kanda ya Mashariki Kusini, Hamad Taimuru, alipofanya ziara ya kukagua ghala la kuhifadhia kemikali aina ya salfa la kampuni ya African Inland Logistics Ltd, Kata ya Sandali, wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Timu ya wataalamu kutengeneza mifumo ya utumishi kidijitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imeunda timu ya wataalamu wabobezi ambao wameanza kutengeneza mifumo mipya ya kielektroniki ya usimamizi wa utendaji kazi wa watumishi wa umma na taasisi za umma.

Sambamba na hilo imeeleza kuwa utekelezaji wa ahadi alizozitoa Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa Sikukuu ya Wafanyakazi mwaka jana, zinaendelea kutekelezwa kwa vitendo ikiwamo ulipaji wa madeni ya mishahara.

Waziri wa ofisi hiyo, Jenista Mhagama, aliyasema hayo jana kwenye kikao kazi kati ya serikali na viongozi wa vyama vya wafanyakazi kuhusu mtazamo wa serikali ya awamu ya sita katika kuimarisha utumishi wa umma, uwajibikaji wa hiari na matumizi ya mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa watumishi wa umma.

Alisema ili kupata mfumo sahihi wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma na taasisi kama ilivyoelekezwa na Rais Samia, ofisi hiyo imeunda timu hiyo.

Alisema mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji kazi kwa Watumishi wa Umma (PEPMIS) unatarajiwa kuanza kufanya kazi Julai mwaka huu ili kuondokana na kero za usimamizi wa utendaji kazi zilizojitokeza katika utekelezaji wa mfumo wa awali wa OPRAS, ambao haukuakisi hali halisi ya utendaji kazi wa watumishi hali iliyoleta hisia za kupendeleana au kuoneana.

"Mfumo mpya wa PEPMIS utakuwa ni wa kielektroniki na utaondokana na matumizi ya makaratasi. Pia utaongeza uwazi katika usimamizi wa watumishi na kuondoa upendeleo na uonevu katika upimaji wa utendaji wa watumishi, utaweka mifumo ya ufuatiliaji wa utendaji kazi wa watumishi kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa na yanayopimika,"alisema.

Mhagama alisema serikali imeanza ujenzi wa Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika ngazi ya taasisi (PIPMIS) ambao utaongeza uwajibikaji katika utekelezaji wa sera, mikakati na vipaumbele vya taasisi, sekta na taifa kulinganisha na kushindanisha utendaji wa taasisi na kutoa tuzo za utendaji mzuri kila mwaka.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Prof.Joyce Ndalichako, alisema kikao hicho kinathibitisha namna ambavyo maelekezo ya Rais yanavyozingatiwa kuhusu ushirikishwaji wa vyama vya wafanyakazi kama wadau muhimu wa maendeleo na uchumi.

Kutokana na hali hiyo, Prof. Ndalichako alivitaka vyama vya wafanyakazi kutoa maoni yao kuhusu matumizi ya mifumo hiyo kwa watumishi ili iwe na tija kwao.

# Mwanasiasa nguli ammwagia sifa Kinana

**Na Richard Makore,** MWANZA

MWANASIASA nguli, Mgana Msindai, amesema kuchaguliwa kwa Abdulrahman Kinana kuwa Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara ni sahihi na atamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuendesha nchi kwa demokrasia na haki.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum nyumbani kwake eneo la Pasiansi jijini Mwanza, Msindai alisema Kinana ni mtu mwema na ambaye anajua siasa za utu, heshima na kuvumiliana.

Msindai mbaye aliwahi kuwa Mbunge Iramba Mashariki kwa miaka 15, alisema anamfahamu Kinana kwa muda mrefu na kwamba Rais Samia akimwamini awe mshauri wake atamsaidia kumaliza makundi ndani ya CCM. Alisema kwa sasa kuna makundi ndani ya CCM pamoja na serikali, kwamba moja ya kazi ya Kinana itakuwa kuhakikisha anayaunganisha na kuwa kitu kimoja.

Kinana alichaguliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu Maalum wa Taifa wa CCM jijini Dodoma kwa kura 1875. Aliwahi pia kuwa Katibu Mkuu wa chama hicho.

Alisema makundi yaliyomo ndani ya CCM yasipounganishwa yanaweza kumkwamisha Rais Samia kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia Watanzania.

Msindai alisema kwa kuwa anamfahamu Kinana vizuri, anaweza kumsaidia Rais Samia katika mambo mengi na hivyo kumfanya apumzike.

"Rais atapumzika sana. Amechagua mtu sahihi kabisa. Mimi namfahamu Kinana ni rafiki yangu wa siku nyingi," alisema.

Kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, Msindai alisema: "Hata kama CCM ingekuwa imefanya mambo mazuri kiasi gani kwa wananchi, isingeweza kupata ushindi wa takribani wabunge wote na madiwani".

Akizungumzia uongozi wa Rais Samia, Msindai alisema anaongoza kwa falsafa ya rangi zake. Alisema falsafa hiyo ni nzuri na watendaji ambao hawaijui wanatakiwa kuijua vinginevyo wakiharibu watafukuzwa kazi.

Kuhusu uongozi wa Hayati John Magufuli, Msindai alisema ulikuwa ni uongozi wa kutumia fimbo, kwamba aliyeharibu alichapwa hatua ambayo ilisaidia kunyoosha mambo.

Aidha, alimwomba Rais Samia kulipa madeni ya wazabuni, kufungua milango ya ajira kwa sekta zote, kudumisha demokrasia na kuweka mkazo katika kilimo.

Alisema akifanya hayo atakuwa amegusa maisha ya wananchi wengi ambao ndiyo wapiga kura katika uchaguzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usalama uwekewe mkazo kunusuru maisha ya watu

**WIKI** hii, wananchi katika jiji la Dar es Salaam walikumbwa na taharuki baada ya kuzagaa kwa mafuta jamii ya petroli katika Bahari ya Hindi, eneo la Feri, yaliyodaiwa kuwa yamemwagwa na meli isiyofahamika huku wananchi waliokuwa katika sehemu hiyo wakiona ni fursa na kuanza kuyachota kwa lengo la kwenda kuyauza.

Mashuhuda wa tukio hilo waliwaambia waandishi wa habari kwamba tukio hilo lilitokea siku moja kabla ya taarifa kuvifikia vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na mamlaka husika, wakiwamo viongozi wa serikali.

Baada ya vijana kuchangamkia suala hilo kama fursa kwao, polisi walifika eneo hilo na kuanza kuwapoka wananchi madumu waliyokuwa wamehifadhi mafuta hayo sambamba na kuwakamata wahusika.

Mmoja wa wananchi waliokuwa katika eneo hilo, alibainisha kuwa wananchi walianza kusikia harufu kali ya mafuta na baada ya hapo watu walianza kukimbilia eneo la ufukweni yalipokuwa yametapakaa na kuanza kuyachota. Kwa mujibu wa shuhuda huyo, mafuta hayo yalionekana kwa wingi wakati bahari ikiwa imejaa.

Ikiwa ni siku ya pili tangu mafuta hayo kuonekana baharini, Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Ngw'ilabuzu Ludigija, ambaye eneo hilo liko chini ya utawala wake, alifika na kuwatahadharisha wananchi kuwa makini na ununuzi wa mafuta ya kidumu kuanzia sasa.

Pia alibainisha kuwa mpaka wakati huo, walikuwa hawajafahamu ni meli ipi ambayo imemwaga mafuta hayo na kwamba wameshatoa maagizo kwa mamlaka mbalimbali kuanza kuchunguza athari za mafuta hayo.

Sambamba na hayo, aliagiza uongozi wa soko la feri, kutotumia maji yenye mafuta hadi hapo uchunguzi utakapofanyika kwa kuwa yanaweza kuwa na athari kwa afya ya binadamu.


Baada ya kauli hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema taasisi yake inatarajia kuanza uchunguzi wa tukio hilo kesho yake kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) na wanaoingiza mafuta ili kubaini aliyefanya uchafuzi huo wa mazingira.

Kuchelewa kubainika kwa mafuta haya kutoka mahali yaliko matangi ya hifadhi au zinakotia nanga meli hadi eneo la Feri, kunatia shaka juu ya utendaji wa baadhi ya taasisi, tunasema hivyo kwa sababu viongozi wametoa taarifa baada ya siku mbili ilhali karibu na eneo hilo kuna polisi wa doria, hivyo wangeng'amua na kutoa taarifa mapema.

Ni vyema vyombo vyetu vilivyopewa dhamana ya udhibiti na usimamizi wa mambo mbalimbali, vikafanya kazi kwa weledi ikiwamo kubaini viashiria vya hatari kwenye maeneo mbalimbali kabla ya kuleta madhara kwa wananchi.

Suala kama la kutapakaa kwa mafuta baharini na wananchi kuanza kuchota ni ishara kwamba kuna ulegevu mahali, hivyo kuna ulazima kwa wahusika kujitafakari na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Viwanda vya kuchakata mboga na matunda vinaweza kuwa mkombozi

**TANZANIA** imejaliwa kuwa na matunda ya aina mbalimbali yakiwamo maparachichi ambayo yanatajwa kuzalishwa kwa wingi nchini na sasa serikali inaandaa mikakati ya nchi kuwa na soko la uhakika la matunda hayo.

Miongoni mwa mikakati hiyo ni kuendelea kufanya mazungumzo na serikali ya Afrika Kusini ili kupata soko ambalo litakuwa na uwezo wa kuchukua maparachichi yanayozalishwa hapa nchini.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, hatua hizo za serikali zitasaidia kutatua kero ya wakulima kuingia hasara kwa kutupa matunda hayo baada ya kuoza, kutokana na kukosa soko.

Ni kauli aliyoitoa wakati akizungumza na wakulima wa Wilaya ya Rungwe mkoani Mbaye, baada ya kutembelea mashamba ya kiwanda cha matunda hayo cha kampuni ya Kuza Afrika Ltd kilichopo katika Kijiji cha Ilolo, Kata ya Kiwira.

Waziri Mkuu anawataka wakulima wa wilaya hiyo na maeneo mengine ambapo maparachichi yanastawi kwa wingi, kuendelea kuzalisha zaidi, kwa kuwa ana uhakika soko lake litapatikana.

Aidha, Wizara ya Kilimo imepewa jukumu la kusimamia kilimo cha matunda hayo na kuwatafutia wakulima mbegu bora, kutunza miche shambani na kutafuta masoko na kuwataka wakulima waongeze kasi ya kilimo.

Anawaagiza maofisa kilimo kuanzia wa mkoa hadi wilaya kuwasaidia wakulima kufanikisha kilimo cha kisasa cha matunda hayo, huku wakurugenzi wakitakiwa kuhakikisha maofisa kilimo kwenda kwa wakulima.

Kimsingi hatua hiyo ni nzuri na inaweza kusaidia wakulima wa matunda hayo kunufaika, hasa kwa kupata soko la uhakika na kuepusha hasara ambayo wamekuwa wakikumbana nayo ya kuoza baada ya kukosa soko.

Juhudi hizo za serikali za kutaka kuwasaidia wakulima wa maparachichi kwa kuwatafutia soko nje ya nchi, ni hatua nzuri, lakini pia si vibaya hamasa ikaelekezwa pia kwenye uwekezaji wa viwanda vya matunda hayo hapa nchini.

Wakati soko likitafutwa nje ya nchi, si vibaya serikali ikahamasisha pia ujenzi wa viwanda vingi zaidi vya kuchakata matunda nchini, ili wakulima wawe na sehemu ya kutosha ya kuuza kuliko kutegemea viwanda vichache vilivyopo.

Ninaamini hatua hiyo inaweza kusaidia kuongeza soko la ndani la matunda ya aina zote badala ya maparachichi, bali pia kwa mananasi, machungwa, maembe na mengine ambayo yamekuwa yakioza kwa kukosa soko.

Hatua hiyo na kuwapo kwa viwanda vingi vya kuchakata matunda, inaweza kusaidia juhudi za serikali za kutaka Tanzania kuingia katika masoko ya kimataifa kwa kuuza bidhaa zinazotokana na matunda yanayopatikana nchini.

Ni kweli serikali inataka nchi ifikie kuwa ya viwanda, nami ninaamini kuwa ikiwa na viwanda vingi vya kuchakata matunda mbalimbali lengo la serikali linaweza kutimia la nchi kuwa ya viwanda.

Kwa nia hiyo ya dhati ya serikali kwa wananchi wake, ni vyema ikaendelea kupanua wigo hasa wa kuwa na soko la uhakika la ndani na nje nchi hasa kupitia viwanda vya kuchakata matunda.

Iwapo viwanda vitakuwa vichache, maana yake ni kwamba matunda yatapelekwa nje na kuchakatwa huko Watanzania wanauziwa juisi inayotokana na matunda wanayolima wenyewe badala ya wao kuchakata na kuuza nje.

uchache wa viwanda vidogo, kwa namna moja au nyingine unachangia wakulima kuendelea kupata hasara, kutokana na ukweli kwamba, hayawezi kukaa muda mrefu bila kuharibika.

Hivyo, ingependeza sana kama suala la kuwapo kwa viwanda vingi vya kuchakata matunda litatiliwa mkazo ili wakulima wapate sehemu ya kwenda kuuza badala kuyachuma na kuyamwaga chini kusubi wateja.

**SAFU**

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Jiandae kustaafu bila kuwa na 'stress' kwa kufanya yafuatayo



Na Pascal Mayalla

IJUMAA ya Aprili 8, mwaka huu, yaani juzi, ilikuwa siku yangu ya kuzaliwa, nikiwa nimepiga mingi karibia miaka 60 ambao ndio umri rasmi wa kustaafu.

Kwa sasa tayari ni baba wa 8 +1= 9, babu wa wajukuu sita na karibu nastaafu.

Shabaha kuu ya makala hii si kusherehekea siku yangu ya kuzaliwa, bali kutoa mbinu za changamoto za ulezi katika umri mkubwa huku unajiandaa kustaafu na vichanga vinaendelea kuzaliwa.

Naomba kutoa taarifa ya ujio wa mgeni mwingine kwenye familia yangu. Ujio wa mgeni huyu umegongana na tarehe yangu ya kuzaliwa. Mgeni huyu mpya amebisha hodi Aprili 8, 2022 majira ya saa 4:00 asubuhi katika hospitali ya Aga Khan. Kwa vile mgeni mwenyewe ni kidume, nimetoa jina langu la Pascal, hivyo ataitwa Pascal Mayalla, Jr. na kuanzia leo mimi nimebadili jina na kuwa Pascal Mayalla Snr baada ya ujio wa Pascal Mayalla Jr.

Kupata mtoto katika umri mkubwa kama huu, kuna changamoto zake. Changamoto ya kwanza, ni watoto wangu wakubwa tayari wana watoto, yaani mimi ni Babu halafu unapata mtoto mdogo kuliko mjukuu. Kwa wajukuu wa watoto wangu wa kiume, huyu Pascal Mayalla Jr. ni baba yao mdogo na wajukuu wa mabinti huyu ni mjomba wao. Baba mdogo na mjomba kuwa ni mdogo kuliko wajukuu, haupendezei kivile!.

Kuna watu wataona ni ajabu kwa mtu wa zaidi ya miaka 50 kiumri kupata mtoto japo ni kweli si kawaida sana. Watu wanajenga familia wakiwa vijana na ukifika miaka 50 ni umri wa kujiandaa kustaafu na si tena kuanza kulea na kuitwa baba wakati umri ni wa babu.

Lakini amini usiamini, kupata mtoto katika umri wa miaka 50 na kuendelea ni kawaida sana. Tuna mifano mingi tu, ukitafuta umri wa Chief Burito wakati Julius Kambarage Nyerere anazaliwa, hutashangaa. Hata Nabii Ibrahim alipomzaa Isaka alikuwa na miaka karibu 100. Mfano mzuri wa karibu ni yule Mzee wetu fulani, al maarufu na mashuhuri, alipata watoto mapacha akiwa na miaka 74. Hivyo mimi kupata mtoto katika umri wa miaka 50 na zaidi ni bado sana lakini huyu ndiye wa mwisho.

Kusudio la makala hii ni kutoa somo la kujiandaa kustaafu ili ustaafu bila kuwa na msongo wa mawazo, wazungu wanasema stress. Kitendo tu cha mstaafu mtarajiwa kupata mtoto akiwa na zaidi ya miaka 50 ya umri, hiyo peke yake tayari ni 'stress' tosha kwa sababu mtoto anatakiwa kutimiza 'the age of majority', akiwa na utegemezi kamili. Pesa za mstaafu, haziwezi kumlipia shule nzuri mtoto, labda nikubali akasome St. Kayumba. Kama hao wenzake wanane hakuna aliyesoma St. Kayumba, hivyo huyu kitinda mimba wa Baba Babu, inatakiwa kwa kiasi kikubwa nijipange zaidi. Kwa hiyo makala hii itakuwa msaada mkubwa sana kwa wale wote wenye umri mkubwa, huku wakikabiliwa na changamoto za ulezi.

Kutokana na maandalizi duni ya kustaafu, wastaafu wengi hujikuta hawana vitega uchumi vya kutosha kuwawezesha kuhimili mikiki ya maisha baada ya kustaafu, hivyo kuishi maisha ya 'stress'.

Wengine husumbua watoto kwa kupiga mizinga, hali inayosababisha ukiona tu simu ya dingi, unahisi ni mzinga. Ukijiona uko apeche alolo, unaogopa hata kupokea simu ya dingi ukidhani ni mzinga kumbe simu nyingine wala si mizinga. Ni dingi amekukumbuka tu na anakupigia ili kukusalimia.

Kitu kinacholeta 'stress' kubwa kwa wastaafu wengi, ni wengi kutofanya biashara yoyote wakati wa utumishi wao halafu wakiisha kustaafu yale malipo ya pensheni ya mkupuo huyatumia kama mtaji wa kuanzisha biashara. Biashara isipokwenda vizuri, matokeo yake ni kupata 'stress', kuchoka mapema na kuchakaa na hapo hapo maradhi ya sonona (depression) na mwisho ni kufa mapema kwa shinikizo la damu, maradhi ya moyo, maumivu ya viungo na kufeli kwa viungo muhimu kama figo na ini.

Ili kuzuia 'stress' za kustaafu, kama unapanga kufanya biashara fulani baada ya kustaafu, anza kidogo kidogo ukingali kazini kupata uzoefu wa kutosha. Ukiona unaweza ndipo ukistaafu ujikite zaidi.

Ushauri wangu wa njia nzuri ya kustaafu ni zile fedha za mafao yako ya kustaafu ambayo umelipwa kupitia benki, wastaafu wengi huziweka fedha hizo benki kama akiba na kuzitumia kidogo kidogo.

Kitendo cha fedha hizo kukaa benki kwenye akaunti ya akiba faida yake ni kiduchu sana. Zingekaa kwenye akaunti ya muda maalum (fixed deposit account) zingezalisha faida kubwa kidogo. Lakini mpango mzima wa ukweli na wa uhakika wa uwekezaji wa mafao yako ni kwa kuwekeza kwa ununuzi wa dhamana za serikali (government bonds) ambazo huuzwa na Benki Kuu ya Tanzania na hutoa riba ya mpaka asilimia 16.

Sasa tupige hesabu ya Pamoja. Tuseme mafao yangu ya kustaafu ya mkupuo ni Sh. milioni 100. Nikinunulia dhamana za serikali za miaka 25, kila mwaka nitapata Sh. milioni 16. Dhamana hizi wanalipa gawio mara mbili kwa mwaka, kila baada ya miezi sita, utalipwa Sh. milioni nane kila miezi sita. Ukiishanunua dhamana hizo, zile stakabadhi ni dhamana ya uhakika ya kupata mkopo benki yoyote kufanyia biashara yoyote.

Nakushauri, fanya utaratibu na benki yako badala ya kusubiri kupokea gawio lako la Sh. milioni 16 kwa mwaka, unaomba ulipwe shilingi milioni 1.3 kila mwezi kwa muda wa miaka 25, bado wewe mstaafu utakuwa na 'stress' au kusumbua kupiga mizinga watoto?

Wastaafu wenzangu watarajiwa, ni muhimu sana kupanga uzazi, ni muhimu kupanga familia, ni muhimu kujipanga kustaafu bila 'stress'. Lakini ikitokea umepata ugeni kama Pascal Mayalla Jr., muda wa machweo, mpokee tu mgeni kwa mtazamo chanya na moyo mkunjufu kwani kila mtoto anakuja na riziki yake,

**Karibu Pascal Mayalla Jr.**

**Happy Born Day Pascal Mayalla Jr. Happy Birthday Pascal Mayalla Snr**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mabadiliko ya tabia za watu yatatufikisha pabaya



Na Joseph Kulangwa

**Lakini tukisimuliwa kwamba watu wa zamani walikuwa miraba minne na nguvu nyingi, ni kwa sababu walikula vyakula vibichi huku wakitembea na kukimbia sana, kila siku kutafuta riziki.**

BINADAMU alipoumbwa na kuamrishwa kudhibiti mazingira aishimo ili kumsababishia maisha, alifanya hivyo bila hiyana, akiishi mapangoni na kula mizizi, matunda na hata baadhi ya majani.

Katika kula mizizi, akagundua vyakula kama mihogo, viazi na karanga, mingine akitumia kama dawa, lakini pia katika kula matunda ndivyo hivyo tena matunda chekwa, na hata majani, ndiyo sababu tunafakamia miwa.

Maisha hayo yaliendelea taratibu, binadamu akibadilika, akiacha kukaa uchi na kuvaa magome ya miti na ngozi za wanyama aliowawinda kwa chakula, hakutofautisha chakula na kitoweo.

Aliendelea kula vyakula hivyo kabla hajajua kupika kwa maana hajagundua moto. Alivifakamia vibichi ikiwa ni pamoja na nyama ya wanyama aliowinda na hakudhurika, ndiyo sababu hakukuwa na hospitali.

Yalipokuja haya tunayoyaita maendeleo, ndipo tukaanza kuambiwa kumbe mbu anaambukiza malaria, kumbe mbung'o anaambukiza malale, kumbe kuna virusi vinasababisha magonjwa mbalimbali.

Zamani hizo nzi hakuwa adui wa binadamu, aliweza kutua kwenye maji au maziwa na akaondolewa na watu wakaendelea kunywa bila kusikia huyu kaharisha au yule kahara damu.

Walipokuja hao tunaowaita wanasayansi, ndipo sasa wakaanza kutukataza kula hiki na kile. Na hapo ni baada ya moto kugunduliwa na hivyo nyama mbichi ikapigwa marufuku kuliwa.

Lakini tukisimuliwa kwamba watu wa zamani walikuwa miraba minne na nguvu nyingi, ni kwa sababu walikula vyakula vibichi huku wakitembea na kukimbia sana, kila siku kutafuta riziki.

Ni nyakati hizo waliua wanyama na kuwatafuna baada ya kuwachuna ngozi kwa kutumia zana zao za enzi hizo zilizotokana na mawe.

Kinachoitwa maendeleo kikaja kutulemaza sasa, watu kusafiri tukataka vyombo vya kusafiria, zikaja baiskeli tukizishangaa, mtu unapandaje chombo chenye tairi mbili na kuondoka nacho!

Lakini ikawa hivyo, tukafurahia kusafiri kilometa hata 100 kwa baiskeli kutoka eneo moja kwenda lingine. Kumbuka wakati wa kuja baiskeli tulishagundua pia kuvaa nguo, vinginevyo hali ingetusuta, unapandaje baiskeli bila nguo.

Mara yakaja magari, mshangao wa kuua mtu, yakinguruma na kutembea kwa tairi nne. Kuna mahali tunasimuliwa, siku ya kwanza kuona gari walichuma nyasi kulipelekea wakidhani linakula kama ng'ombe.

Baadaye, tukaacha kula viporo asubuhi na kuanza kuchemsha chai na uji, eti kifungua kinywa. Tofauti kabisa na tulivyosimuliwa na mababu wa mababu zetu, kuwa mtu aliamka asubuhi akakamata kiazi au mhogo wa jana maisha yakasonga.

Tukaendelea kubadilika na mara tukaanza kutafuta eti mafuta kwa ajili ya kupikia, kwamba bila mafuta hakuna chakula kinachopikwa. Tukakamua nafaka na kutoa mafuta tukayatumia kupikia.

Baadhi ya wanyama kama mbuzi na kondoo na hata nguruwe wakawa wanajikaanga kwa mafuta yao wenyewe. Maisha yakawa ya mafuta ya nazi, michikichi, alizeti, karanga, ufuta, na kadhalika.

Huo ukawa ndio ulemavu wetu, tukalemaa, kila mama alipotaka kupika sharti amtume mwanawe dukani akanunue kibaba cha mafuta ya nazi, pamba au karanga, ili mradi tu samaki apikwe siku hiyo.

Mafuta yakawa ndugu kabisa na mchele, kwamba wali au pilau hailiki bila mafuta. Tukazoea, ikawa sehemu ya maisha yetu, watu wakasahau chukuchuku, wakadharau mchemsho.

Leo tunahaha, mafuta yanapanda bei tunaachama na kutoa vilio. Tunaangalia juu mbinguni kumwomba Mungu eti hilo janga liondoke. Janga la mafuta ya kula kukosekana na yakipatikana bei juu.

Tunalaani vita vya Russia na Ukraine eti si tu kuwa vinapora maisha ya binadamu wenzetu, lakini vimesababisha uhaba wa mafuta yatokanayo na alizeti yanayozalishwa kwa wingi Ukraine.

Tunalia eti hivi sasa hakuna ngano, hivyo tutakosa mikate kwa ajili ya kifungua kinywa asubuhi na wengine chakula cha mchana na hata chajioni.

Uzwazwa gani huu umetukumba sisi Watanzania, hivi ni lazima kupika chakula kwa mafuta? Kwani bila mafuta chakula hicho hakitafuniki hakimezeki? Hivi hatuwezi kula muhogo au viazi asubuhi kwa chai, lazima mikate, chapati na maandazi?

Hivi tunalia nauli zitapanda, tunashindwa kukanyaga kwa mguu kwenda huko twendako kama walivyofanya zamani wazee wetu? Kwanza wataalamu wanatwambia kutembea ni mazoezi na kupunguza kama si kuacha mafuta ni afya. Mpo?

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Tume Huru Uchaguzi ianze halafu Katiba mpya ifuate



Na Thobias Mwanakatwe

KUMEKUWA na mjadala kwa muda mrefu kwa wanasiasa ambao wanaishinikiza serikali kuanzisha mchakato wa kupata Katiba mpya.

Lakini pia wengi tumekuwa tukisoma au kusikia Katiba. Zaidi ya hayo, wengi tukadhani neno au dhana hii haituhusu bali ni maalumu kwa wanasheria au wasomi tu. Ukweli ni kwamba, Katiba ni kitu muhimu mno.

Kama msingi ulivyo na umuhimu katika ujenzi wa nyumba, kadhalika na Katiba ni muhimu sana kwa taifa na watu wake. Pia ina uhusiano wa moja kwa moja na maisha yetu ya kila siku.

Kwanza, safari ya mchakato wa kupata katiba mpya ulianza tangu mwaka 2010, wakati Rais wa wakati huo, Jakaya Kikwete, alipoamua kuutangazia umma dhamira na nia ya serikali ya kuanzisha mchakato wa kupata Katiba mpya.

Mchakato ukaanza rasmi mwaka 2011 kwa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83 ya mwaka 2011 na baadaye ikatungwa Sheria nyingine ya Kura ya Maoni Na. 11/2013.

Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ilitamka kuanzishwa kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilianzishwa chini ya Waziri Mkuu wa zamani, Jaji Joseph Warioba, ikaratibu mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi na kuandaa rasimu ya kwanza ya katiba ambayo kupitia uhariri wa Mabaraza ya Katiba ikapatikana Rasimu ya Pili ya Katiba.

Rasimu hii ya pili ambayo ni maarufu kama Rasimu ya Warioba ikawasilishwa kwenye Bunge Maalum la Katiba (BMK) ambalo kwa kiasi kikubwa lilikuwa na wajumbe wengi kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Kwenye bunge la Katiba, ambalo Makamu Mweyekiti wake alikuwa Samia Suluhu Hassan ambaye kwa sasa ndiye Rais wa Tanzania, kuliibuka mivutano mikali kuhusu masuala kadhaa yaliyomo kwenye katiba ilipoanzia. Hatua hiyo ilisababisha baadhi ya wajumbe wa Bunge la Katiba hasa kutoka upinzani, kujitoa na kususia mchakato, waliobaki waliendela na ikapatikana Katiba Pendekezwa ambayo wengi waliiona kama imekosa mwafaka na maridhiano ambayo yanaonekana kama ndio msingi wa kupata Katiba bora ya kitaifa yenye kukubalika na wengi.

Ilipofika uongozi wa serikali ya awamu ya tano, vuguvugu la kudai Katiba mpya lilianza ambalo limeendelea kwa kasi kipindi hiki cha serikali ya awamu ya sita, vyama kadhaa vya siasa vimetoa matamko ya kutaka mchakato uanze.

Hata hivyo, Rais Samia Suluhu Hassan alishatoa msimamo wa serikali kwamba suala la katiba mpya lisubiri kwanza ili serikali yake iweke nguvu katika kujenga nchi kiuchumi. Licha ya tamko hilo la mkuu wa nchi, bado viongozi wa vyama vya siasa wameendelea kupaza sauti wakitaka katiba mpya.

Kwa upande wangu pamoja na wadau wengine wa siasa akiwano Katibu Mkuu wa CCK, Renatus Muabhi, tunahoji hivi kipi kinapaswa kuanza kutekelezwa kati ya Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

Kimsingi, kwa maoni yangu naona kinachotakiwa kuanza kufanyika ni kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi kwa sababu ambazo nitazielezea hapa chini.Wanasiasa na wadau wote wa kisiasa walione suala la kuwa na tume huru ya uchaguzi liwe ndilo kipaumbele namba moja kwa sababu ikipatikana itaharakisha upatikanaji wa katiba mpya kupitia wingi wa wabunge katika bunge ambacho ndio chombo kinachoweza kuisimamia serikali kwenye uanzishaji katiba mpya.

Huwa nawashangaa ninapowaona baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa wanasema hawaoni umuhimu wa tume huru ya uchaguzi kabla ya katiba mpya wakiamini katiba hiyo ndiyo inaweza kuvunja aina ya mifumo ya uchaguzi iliyopo hapa nchini wakati si kweli.

Katika mazingira kama haya ya kisiasa tuliyonayo hatuwezi kukaa na kuona kwamba katiba ni muhimu kuliko tume huru ya uchaguzi ambayo ndio inasimamia haki na misingi yote ya amani na utulivu.

Wanasiasa watambue kuwa Tume ya Uchaguzi ndiyo yenye kutoa uamuzi na kutangaza nafasi zote za uongozi wa kisiasa kuanzia ngazi ya chini hadi ya rais,kwa hiyo utekelezwaji wa haki na amani imebebwa kwa asilimia 80 na kutokuwa na tume huru ya uchaguzi kwa sababu hapo ndio 'reaction' ya machafuko yanapoweza kuanza.

Viongozi wa vyama vya siasa, wafuasi na wanachama wao inapofika wakati wa uchaguzi mkuu ambao husimamiwa na Tume ya Uchaguzi huwa wakiamini watafanya vizuri katika uchaguzi husika lakini matokeo yanapotangazwa na kuwa tofauti na matarajio yao, wanaelekeza lawama kwa tume na hapo ndipo unakuja kuona umuhimu wa Tume Huru ya Uchaguzi kuliko katiba mpya.

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com au 0692-276999**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

## DARASA LA NDOA

# TOFAUTI KISAIKOLOJIA ZINAVYOWEZA KUIMARISHA AU KUBOMOA UHUSIANO



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

MOJA ya sababu za migogoro na kuvunjika kwa ndoa nyingi ni kukosa ufahamu kuhusu tofauti zilizopo kati ya mwanamume na mwanamke. Lakini wanandoa wanapofahamu tofauti walizo nazo itawasaidia kujua namna ya kuchukuliana katika mazuri na udhaifu wao.

Hatua hii itasaidia kuwa na uhusiano bora na wenye mafanikio. Hali kadhalika, ufahamu huu utawasaidia wanaume na wanawake wote kujua namna ya kuheshimiana na kuishi pamoja kwa amani na utulivu katika jamii na maeneo yao ya kazi.

Tofauti zilizopo baina ya mwanamke na mwanamume huathiri mtazamo na mwenendo wao. Tofauti hizo zinaweza kutokana na utamaduni, mazingira na mwingiliano wa kijamii na iwapo zitatumika vizuri huleta manufaa na zisipozingatiwa zinaweza kuwa chanzo cha migogoro katika ndoa, maeneo ya kazi na jamii kwa ujumla.

Zifuatazo ni tofauti zilizopo kisaikolojia kati ya jinsi hizo mbili:

**Wanawake**

Wanawake ni watu wepesi na wana uwezo mkubwa wa kuanzisha uhusiano bora na hali hii imewafanya kuwa mstari wa mbele na kuelekeza nguvu zao katika masuala mengi ya kifamilia na kijamii. Kwa sehemu kubwa, wanawake ndio wenye muda zaidi na wazazi wa watoto wao kuliko wanaume.

Aidha, wanawake ni watu wanaopenda kuongea, hivyo, hukabili matatizo kwa kuongea. Kwa kuwa wanawake wanapenda kuongea, huhitaji mtu wa kuwasikiliza kwa dhati na upendo. Itokeapo changamoto ya kiuhusiano, wanawake wengi ni wepesi wa kuongea maneno mengi na kumshirikisha mtu mwingine mambo yake ikiwa ni sehemu ya kutafuta suluhu na faraja.

Jambo lingine ni kwamba wanawake huongozwa na hisia (emotions) zaidi kuliko mantiki (logic) na kwa sababu hiyo hakuna jambo dogo kwao. Jambo ambalo mwanamume anaona ni dogo, kwa mwanamke ni kubwa. Kwa mantiki hiyo, usishangae sana kuona mke kabeba begi la nguo zake na kuondoka nyumbani kwake baada ya kugombana na mume wake. Hii ni moja ya sababu zilizofanya Maandiko Matakatifu ya Mungu kuwataka wanaume waishi na wake zao kwa akili, hivyo wanaume wasipuuzie hisia za wanawake kwani huweza kuleta athari kubwa katika uhusiano na maisha.

Wanawake wana uwezo wa kuona na kugundua hatari kwa haraka. Kwa maneno mengine, wana jicho la tatu. Zaidi ya hayo, wanawake hupenda kujua undani wa mtu, hali ambayo hupelekea wanawake wengi kuwa wadadisi wa mambo.

Kadhalika, wanawake huvutiwa na habari na masimulizi kuhusu watu, hivyo, si jambo la ajabu kuona wanawake wakitumia muda wao kumzungumzia mtu au watu na kuamini kwa wepesi jambo wanaloambiwa na mtu mwingine. Hata hivyo, haishauriwi kuamini kila jambo linaloelezwa na mtu kwani huwezi kujua lengo la mtoa habari. Ni muhimu kujipa muda wa kuchunguza ili kufahamu ukweli wa jambo mtu analoambiwa kabla ya kufanya uamuzi au kuamini.

Uhusiano wa watu wengi umevurugika kwa sababu ya watu kuamini na kuyafanyia kazi mambo ya kuambiwa yasiyo na ukweli. Hali hii imesababisha maumivu na majeraha ya nafsi kwa watu wasio na hatia.

**Wanaume**

Mwelekeo mkubwa wa wanaume hauko katika watu, bali vitu na majukumu na hii ndiyo sababu mojawapo ambayo imefanya wanaume wengi kueleekeza nguvu zao katika kazi zaidi kuliko mambo ya nyumbani au familia. Hali hii inahusishwa na wajibu mkubwa walionao wanaume wa kuhangaikia mahitaji ya familia zao. Hata hivyo, hicho kisiwe kisingizio cha kudumu kwa kinababa kukosa muda na familia.

Wanaume si wepesi wa kusema mambo yao bali hupenda kunyamaza. Kuna msemo kwamba wako tayari kufa na tai shingoni kwa sababu ya hulka ya kupenda kutatua matatizo kwa vitendo na hoja. Mara nyingi itokeapo hali ya mgongano ndani ya ndoa, wengi wao hupenda hunyamaza kimya na kuchukua hatua kimya kimya kama njia ya kutafuta suluhu ya tatizo, hata kama hatua hizo hazina manufaa kwa familia na uhusiano wao.

Pia wanaume ni wepesi wa kuanzisha uhusiano mwingine nje ya ndoa pale unapotokea mgogoro wa kiuhusiano. Hali kadhalika, wako wanaume ambao ni wepesi sana wa kuchukua hatua ya kuwapiga wake zao kama sehemu ya kutatua tatizo, jambo ambalo ni kosa la jinai.

Kwa mantiki hiyo, wanawake wasipende kuzozana na kujibizana na waume zao kwa kuwa hali hiyo huchochea hasira za mwanamume na huweza kuleta madhara makubwa. Mwanamume hupenda kukosolewa kwa staha na si kwa majibizano. Siku zote hakuna mwanaume mkorofi mbele ya mwanamke mnyenyekevu.

Tofauti nyingine ya kisaikolojia ni kwamba wanaume huongozwa na mantiki zaidi kuliko hisia. Hali hii imesababisha wanaume wengi kutokupenda kutoa itikio la haraka katika jambo husika kwa sababu ya hulka ya kutaka kupata muda wa tafakuri. Kwa hiyo, mke anapohitaji jambo fulani kutoka kwa mume wake, wakati mwingine asitegemee kupata majibu ya haraka au utekelezaji wa papo kwa papo.

Wanaume huvutiwa na ukweli (facts) wa masuala (issues) na data kwa ajili ya uthibitisho. Hali hii ndiyo inayosababisha wanaume wengi kutokuwa wepesi wa kuamini mambo au jambo kwa haraka. Kinyume cha hapo, mwanamume huyo atakuwa na vinasaba vya tabia za kike.

Hata hivyo, ieleweke kwamba hakuna binadamu mkamilifu. Kila binadamu ana mazuri na mabaya yake. Jambo la msingi ni kwamba wanandoa wafahamiane, wasaidiane, wakosoane kwa staha kwa sababu kukosoana si dalili ya udhaifu bali kujali. Pia wanandoa wajifunze kuvumiliana, waelekezane na kuimarishana kwa upendo na upole ili kujenga ndoa na familia bora.

- **Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz.**

**Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

APRILI 10, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili




Ukurasa 14

## Utamu wa vipapatio vya kuku




Ukurasa 13

## MITINDO

UBEBAJI MIKOBA

Mitindo inayowalewesha wanawake




## KATUNIKA


Ukurasa 16




# FURAHIA
## urembo wa kucha

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA







| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | P | A | M | B | A |
| ■ | E | ■ | ■ | A | ■ |
| A | P | A | ■ | N | ■ |
| ■ | O | ■ | O | G | A |
| ■ | N | ■ | ■ | U | ■ |
| L | E | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI

TAFUTA NJIA KUANZIA ALAMA A HADI Z




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
ODA, OKA, BANDA, TAMBO, BANDUA, TAKASA

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

Hivi ndivyo watoto wanavyotofautiana kati ya nchi mbalimbali duniani

Marekani mtoto anapoenda kulala anamwambia mama yake "usiku mwema mama"

Uingereza mtoto humuambia mama yake "Ndoto njema mama"

Uhispania wanapoenda kulala humtakia wazazi "usiku mwema wazazi wangu wapendwa"

Tanzania mtoto anapokwenda kulala utamsikia "Mama kaniwekee neti nasikia usingizi,"

**SWALI**

Nyumbu wanaohama kila msimu wanapatikana mbuga gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Imani inavyoweza kukupatia muujiza ulio mbele yako

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vyetu vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tuangalie imani inavyoweza kufanikisha malengo yako kimaisha.

Ukiamini kwamba utafanikiwa, ni kweli utafanikiwa. Na ukiamini kwamba utashindwa, utashindwa kweli. Imani ni rahisi kiasi hicho lakini wengi wameshindwa kutumia nguvu ya imani kujiletea mafanikio.

Moja ya maandiko ya Mungu linasema, "Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana". Hapa ikimaanisha kwamba imani ni uhakika wa kuona yale yasiyoonekana kwa macho.

Maono hupokelewa kwa imani, na ndiyo macho yatakayo kuwezesha kuyaona maono ya Mungu kwa ajili yako. Ratiba ya maono yako huko mbinguni imekwisha kutayarishwa mpaka mwisho. Mafanikio yako tayari yamekwishatukia na kilichobaki ni kujidhihirisha kwako.

Imani ndio chombo kitakachowezesha kufanikisha maono yako hapa duniani. Hakuna maono ambayo Mungu amewatayarishia wanadamu halafu yashindikane huko mbinguni, kwani yanashindikana hapa duniani tu!

Katika ulimwengu wa roho mafanikio yako yapo tayari na imani ndiyo chombo pekee kitakacho kuwezesha kuyapokea. Wengi wetu tumeshindwa kutimiza malengo yetu kwa sababu tunaenenda kwa jinsi ya mwili, tunataka kuona kwanza, kugusa na kuhakikisha kabla hatujachukua hatua ya utendaji.

Imani yetu imejengwa katika yale tunayoyaona na kuyasikia kwa jinsi ya mwili, hatumwamini Mungu hata kidogo! Kama ulimwona mwenzako ameshindwa na kupata hasara katika mradi wake, hata Mungu akuhakikishie vipi kwamba wewe hautashindwa, hautaamini kwa sababu imani yako imejengwa katika kuona kwa jinsi ya mwili.

Tumetumainia sana hekima za kidunia na sio imani katika uwezo wa Mungu. Leo tunafurahia taa za umeme kila mahali kwa sababu Thomas Edison aliona kwa macho ya rohoni kwamba japo kwa sasa hajafanikiwa lakini ipo siku atatengeneza taa ya umeme. Ilimchukua majaribio elfu moja na ndipo alipofanikiwa.

Michael Jordan, mchezaji maarufu wa mpira wa kikapu duniani alipoulizwa siri ya mafanikio yake, alisema ni kwa sababu alishindwa mara nyingi na hiyo ikamwezesha kufanikiwa!

Huwezi kuwa kama Michael Jordan na Thomas Edison kama huna imani ambayo macho ya kiroho yanayokuonyesha mafanikio yako hata kabla hayajatokea. Ukishayaona mafanikio yako katika ulimwengu wa roho, utakaza mwendo na kukataa kuyumbishwa mpaka ufanikiwe.

Hata mtu mmoja aitwaye Bartimayo alikuwa kipofu kwa jinsi ya mwili lakini macho yake ya rohoni yalikuwa yanaona vizuri. Imani ambayo ndiyo macho yako ya kiroho, hukuonyesha kile ambacho Mungu amekusudia kwa ajili yako. Imani hiyo ndiyo iliyompa Bartimayo hitaji kuu la moyo wake!

Mpenzi msomaji, baada ya utangulizi huo, hebu sasa imani ambayo ni macho yako ya kiroho inapatikanaje? Chanzo cha imani ni kumwamini Mungu. Huwezi kumwamini Mungu mpaka kwanza uamini kwamba yupo na ndiye akupaye thawabu!

Ili uweze kumwamini Mungu ni lazima Umwombe Mungu akuwezeshe kumwamini. Hutamwamini Mungu kwa sababu tu tumeamua kumwamini. Imani huumbwa ndani yetu na Roho Mtakatifu kwa wale wenye kiu hiyo. Hapa nazungumzia imani ile itendayo kazi, izaayo matunda.

Kuamini kwamba Mungu yupo inawezekana kuwa ni jambo la kawaida kwa sababu karibu kila mtu anasema anamwamini Mungu. Hebu sikia neno hili la Mungu linavyosema: "Wewe waamini ya kuwa Mungu ni mmoja; watenda vema, mashetani nao waamini na kutetemeka".

Imani yako lazima iwe zaidi ya hawa mashetani, uwe na imani isiyoyumbishwa na dhoruba yoyote. Kipimo sahihi kitaonekana katika mwenendo wako. Je, biashara yako inapoyumba, huduma yako au miradi yako inapokwama unaendelea kumwamini Mungu? Je, macho yako ya kiroho yanaendelea kuona yale maono ya Mungu kwa ajili yako?

Je, unaweza kusema, Piga ua, garagaza chini, na chukua vyote sitaacha kumwamini na kumtegemea Mungu. Kwa kadiri utakavyoendelea kuyaona yale yasiyoonekana kwa macho ya kawaida, imani yako itabaki imara hata upite katika dhuruba gani na siku moja Mungu atakufanikisha.

***Mpenzi msomaji wangu, bila shaka umepata mwanga kidogo kuhusu namna imani ambayo ni macho yako ya kiroho inavyopatikana. Wiki ijayo nichachambua zaidi eneo hilo. Kwa maoni, kisa cha kimaisha tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# Wananchi waelimishwe kuishi kwa mabadiliko ya kiuchumi

MAFUTA ya petroli, dizeli na ya taa yamepanda bei kiasi cha kusababisha bidhaa zingine zote kupanda bei, huku viwango vya mishahara na stahili zingine zikiwa ni zile zile.

Sababu kubwa ya kupaa kwa bei hizo ni kutokana na vita vya Ukraine na Russia kutokana ba ukweli kuwa nchi mojawapo ni wazalishaji wakuu wa bidhaa hiyo muhimu.

Unapokwenda dukani kwa sasa, kila bidhaa imepanda hata kama mzigo uliagizwa zamani kabla ya mafuta kupanda, jambo linaloonyesha kuwa wafanyabiashara wanalenga kupata faida kubwa zaidi kuliko kuwaangalia wananchi wa kawaida.

Kwa sasa sadolini ya vitunguu imefikia Sh. 15,000 kutoka Sh. 5,000 huku bidhaa zingine nazo zikiwa na hali kama hiyo hiyo jambo linalotaka utayari wa kupokea hali hiyo ya mabadiliko kiuchumi.

Tayari serikali imeonya wafanyabiashara waliopandisha bei kupita kiasi jambo linaloumiza wananchi hasa kwenye bidhaa za ujenzi kama nondo ambazo bei yake imezidi kupaa kwa kiasi kikubwa.

Natambua soko huria ambalo hushindana kulingana na hali ya upatikanaji wa bidhaa husika, hivyo atakayepandisha zaidi atakosa wateja kwa kuwa wengi watakimbilia kwa anayeuza kwa bei ya chini zaidi.

Lazima wananchi waelimishwe kupitia vyombo vya habari kuwafikia wananchi kuwapa elimu ya namna ya kujipanga kwa kipato kidogo walichonacho,au kuendelea kuishi maisha mazuri pasipo kikwazo licha ya mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza duniani.

Aidha, wengine walipandisha kwa kisingizio cha UVIKO-19, licha ya serikali kutoa onyo mara kadhaa ikiwamo kufanya tathmini ya bei za bidhaa hizo, lakini bado zilizidi kupanda.

Mathalani, vifaa vya ujenzi vilizidi kupanda bei kabla ya vita, mfano nondo ya milimita 12 ilitoka Sh. 19,500 hadi 26,000, misumari kitoka Sh. 3,000 hadi 3,500, huku sababu kubwa ikiwa ni kupanda kwa bei ya chuma.

Pia, mafuta ya kula ya alizeti yalianza kuadimika na baadaye kupanda bei kutoka Sh. 4,500 lita moja hadi sasa ni Sh. 10,000, huku sabuni ya mche ikipanda kutoka Sh. 2,500 hadi 3,500.

Bidhaa nyingine ni gesi ambayo ilipanda toka Sh. 45,000 mtungi wa kilo 30 hadi Sh. 55,000, hali iliyowalazimu wananchi wengi kurudi kwenye kutumia mkaa au kupandisha bei ya vitafunwa.

Kwa sasa rasmi bei mpya ambazo zimepanda kwa kiasi kikubwa katika historia ya Tanzania, maana yake hakuna namna ya kuzuia kupaa kwa bidhaa hiyo.

Kwa ujumla, kauli za serikali kuwataka wafanyabiashara kushusha bei za bidhaa mara kadhaa, lakini imekuwa ngumu kutekelezwa kutokana na ukweli kuwa ni soko huria na kwamba wauzaji watashindana kwa kadri ya hali ya soko.

Februari, mwaka huu, Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, ilifanya tathmini ya hali ya bei ya bidhaa na kuelekeza wafanyabiashara kutopandisha bei huku ikiahadi kuchukua hatua kali.

Tunatambua wizarani kuna idara ya biashara, ambayo hufuatilia bei za bidhaa kila siku kwenye mikoa mbalimbali na kutoa taarifa, lakini bado haijasaidia kupunguza bei.

Tanzania kuna wasomi wengi wa uchumi wanaoweza kushauri nini kifanyike kuwapunguzia wananchi makali ya maisha, bila kulazimisha wafanyabiashara ambao wana wajibu wa kulipa kodi kupunguza makali.

Kwa nchi zilizoendelea serikali huweka ruzuku kwenye bidhaa, ili kuwasaidia wananchi wasiumie na wauzaji wasipate hasara, lakini kwa nchi zetu ni ngumu zaidi ya kufuatilia kwa karibu hali ya soko ili kuona kama bei si ya maumivu.

Ni lazima serikali ifuatilie kwa karibu hali kwenye masoko na maduka, ili kuona bei zinaendana na uhalisia, kwa kuwa wakiachwa kuna uwezekano wa wafanyabishara kujipanga kuwa na msimamo wa bei ambao unawatengenezea faida kubwa, huku ikiamsha umuhimu wa kuwa na umoja wa walaji ili kutetea maslahi ya wengi.

Pia ni muhimu serikali kufuatilia suala la mishahara ni muhimu likaangaliwa kwa kuwa nayo inapaswa kubadilika kutoka a na mabadiliko yaliyopo ili kuendana na hali ya kiuchumi.

Wananchi wanahitaji kuelimishwa namna ya kuishi kwa hali ya mabadiliko ya kiuchumi,wapo ambao wanachanganyikiwa au kuathirika kisaikolojia kutokana na changamoto za maisha huku tena wanakutana na kupanda kwa bei za mafuta zitakazopandisha bei ya kila kitu.





Dunia inakwenda kwa kasi na kusababisha kila kitu kubadilika kwenda na wakati. Mavazi ya harusi nayo yanaenda kisasa zaidi, pichani ni baadhi ya nguo za harusi kwa wanaume zilizobuniwa katika hali ya kisasa zaidi.

# MITINDO








# UBEBAJI MIKOBA

## MITINDO INAYOWALEWESHA WANAWAKE

MIKOBA ni moja ya pambo linalomng'arisha mwanamke wa kisasa anayethamini mitindo ya kimaisha.

Mitindo ya ubebaji wa mikoba inamwongezea mtu uimara na kujiamini zaidi pale anapokuwa matembezi.

Idadi ya wanawake wanaobeba mikoba inazidi kuongezeka na kusababisha wabunifu kuongeza juhudi ya kutengeneza mitindo mipya aina mbalimbali ya mikoba.

Hata hivyo, wengi hawajui jinsi ya kuitimua kikamilifu kwa lengo la kuongeza mvuto na mwonekano wa kipekee.

Wataalamu wa mitindo wanasema mwanamke ameumbwa katika urembo, hivyo anaweza kupangilia vyema mavazi na mapambo katika kiwango anachopenda.

Chagua mikoba sahihi

Chagua mikoba yenye ubora na gharama unayomudu, muhimu kuangalia ni uimara na malighafi iliyotumika kama unaweza kutumia kwa muda mrefu.

Rangi ya mikoba ilingane na mavazi

Wengi hawajatambua umuhimu wa rangi katika matumizi ya mikoba, hakikisha unakuwa na mikoba ya rangi tofauti kulingana na aina ya mavazi yako. Tabia ya 'kumechisha' inamfanya mtu kuonekana tofauti na nadhifu.

Nunua kwa mahitaji pekee

Hakikisha unanunua mabegi kulingana na mahitaji yako, usinunue kwa wingi na kuyaacha yakiwa hayatumiki, huo ni ufujaji wa pesa.

Mikoba ilingane na umbo lako

Mikoba lazima ilingane na umbo lako, kitaalamu unashauriwa kabla ya kununua angalia umbo lako kwanza kama wewe ni mrefu, mfupi, mwembamba au mnene. Kila aina ya umbo unatakiwa kubeba mkoba unaolingana , mfano ukiwa mrefu na mwembamba unatakiwa kuwa na mikoba ya umbo la duara wenye mikanda mirefu.

URembo

**Na Mary Geofrey**

# FURAHIA urembo wa kucha



KILA siku ubunifu katika suala la urembo linazidi kukua, kila kitu kinabadilika kutokana na kasi ya maisha.

Mabadiliko hayo yamefanya hata urembo wa kucha kwenda kisasa zaidi, imefikia wakati sasa mwanamke mwenye kucha ndefu zilizopakwa rangi ndiye mwenye sifa ya unadhifu.

Kadhalika kucha ndefu humfanya mwanamke awe na ujasiri wakati akizungumza.

Hakikisha kucha zako zinakuwa safi wakati wote na zikianza kubanduka ziondoe na kuweka nyingine.

Wabunifu wamekuwa wakitafuta mbadala wa watu wasioweza kufuga kucha na kupendeza waweze kufurahia kucha zao.

Kuna aina mbalimbali za kupendezesha kucha, ila tutaangalia juu ya ubandikaji kucha, ambao umekuwa ukishamiri kila kukicha hasa kwa upande wa wanawake.

Ubandikaji kucha umekuwa ukifanyika kwa aina tofauti tofauti.

Ila cha msingi ni kutambua unapenda kucha zako ziwe katika muonekano gani, pia tambua rangi itakayo weza kuendana na ngozi yako ya kucha ili uvutie zaidi.

Unashauriwa kujua ni aina gani ya gundi itakayotumika kuwekwa katika kucha ili usipate madhara.

Wakati wakutoa hakikisha unaweka mikono yako yenye kucha hizo bandika katika maji ya uvuguvugu na kubandua taratibu ili usipate madhara.

MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Utamu wa vipapatio vya kuku

VIPAPATIO vya kuku maarufu kama 'Chicken wings' ni mlo unaopikwa kwa ustadi na unapendwa kuliwa wakati wa jioni.

Katika matayarisho yake, kwanza vipapatio vinachovya kwenye mayai kisha kukaangwa kwa muda mfupi kwenye siagi.

Baada ya kukaanga vinachovywa kwenye sauce na kisha kuokwa.

Zikiiva utapata ladha tamu ya chicken wings laini.

Mahitaji

Vipapatio vya kuku kilo moja, yai moja na pasua na vuruga, kikombe kimoja cha unga wa ngano, kwa kuweka utando (layer) juu ya kuku, kikombe kimoja cha siagi (butter).

Mahitaji mengine ni vijiko vitatu vikubwa vya soy sauce, vijiko vitatu, vikubwa vya maji safi na salama, kikombe kimoja cha sukari, nusu kikombe cha white vinegar, kijiko kidogo cha kitunguu saumu cha unga na kijiko kimoja kidogo cha chumvi.

Washa oven kwenye nyuzi joto 350, acha vikauke kwa moto.

Kata vipapatio vya kuku katikati, chovya kwenye mayai na kisha chovya kwenye unga. Hakikisha mayai na unga vimeenea vizuri.

Bandika chombo jikoni kwenye moto wa wastani, acha kipate moto kisha weka siagi. Weka vipapatio ya kuku na kaanga hadi vibadilike rangi. Epua na weka kwenye waya wa kuokea.

Kwenye bakuli ya wastani, changanya soy sauce, maji, sukari, vinegar, kitunguu saumu, na chumvi. Koroga vizuri hadi mchanganyiko uwe sawia. Nyunyizia sauce juu ya vipapatio vya kuku.

Weka vipapatio kwenye oveni, oka kwa muda wa dakika 30 au 45. Weka sauce juu ya vipapatio mara kwa mara. Vikiiva epua na weka pembeni.

Jirambe na ladha tamu ya Japanese chicken wings.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Hizi ndizo kero sugu za madalali kwa wapangaji

## Jinsi ya kupangilia meza ya chai



NDANI ya nyumba kunatakiwa kuwepo na kitu maalum kwa ajili ya kuweka hali ya utulivu zaidi. Moja ya vitu muhimu ni kuandaa meza ya chai nyakati za jioni kwa ajili ya watu kupata kiburudisho kabla ya chakula cha usiku.

Hizi ni baadhi ya dondoo muhimu za jinsi ya kuandaa meza maalum ya chai ndani ya nyumba.

1: Meza ya chakula unaweza kuigeuza kama maalum kwa chai kwa kuweka kitambaa kikubwa kinachofunika meza yote.
2. Weka vikombe vinavyotosheleza kila mahali, pia kuwepo na vitambaa, kulia sahani na kushoto uma.
3. Katikati ya meza weka biskuti, chombo na jam, korosho na maziwa.
4. Vyombo vya kuwekea chai kama chupa huwekwa karibu na mtu atakayehudumia.
5 Ikumbukwe kwamba wanawake hupewa kikombe cha chai na kisosi, kwa wanaume ni kikombe cha chai pekee.

NI kawaida watu wengi wanapokuwa wanatafuta nyumba kwa ajili ya kupanga kwa matumizi ya makazi, biashara au kununua, hutumia madalali ambao ni wabobezi katika eneo hilo.

Pamoja na kupendelea kuwatumia madalali hao, wengi wao wamekuwa wakiwalalamikia kwamba wanawakera. Leo tunaangazia sauti za watu hao ambao wanalalamikia kero wanazokutana nazo kwa madalali hao.

Wa kwanza anasema: "Kiukweli nakerwa sana na madalali wa nyumba za kupanga. Kwanza nataka kujua hii sheria yao ya kuwapa kodi ya mwezi mmoja wanapokutafutia nyumba imepitishwa na nani na je, wanalipa kodi kwa serikali tunayoowapa hiyo kodi ya mwezi mmoja?

"Na hii sheria ya kupelekwa kwenda kuona nyumba au chumba kwa Sh. 5,000 au 10,000 nani kaipitisha? Nimeandika hivi kwa sababu usumbufu tunaoupata wakati wa kutafuta nyumba ni mkubwa mno. Madalali wengine ndio wamekuwa kama wenye nyumba, hadi bei za nyumba wanabadilisha.

"Wanawashauri wenye nyumba kubadilisha au kuongeza kodi ili wapate fedha kubwa. Ikumbukwe kwamba dalali ni daraja la watu wawili, mwenye nyumba na mpangaji lakini inakuwaje jukumu la kulipa hiyo fedha ya mwezi mmoja lisiwe la wote wawili? Kwa nini aachiwe mpangaji peke yake?

"Au walipe wenye nyumba tu na si wapangaji maana wao wanahangaika sehemu ya kujihifadhi. Maskini ya Mungu unakuta alikotoka amefukuzwa kwa kushindwa kulipa kodi ila cha ajabu zaidi anakoenda anatakiwa alipe kodi ya miezi mitatu hadi sita na kodi ya dalali juu pamoja na Sh. 5,000 au 10,000 kila nyumba anayopelekwa kuiona."


Mwingine anasema miongoni mwa kero zinazomtesa kutoka kwa madalali ni kutokupenda kusema ukweli.

"Lipo tatizo la uongo kwa madalali wengi. Unamweleza kwamba nataka nyumba ya aina fulani, anakuambia njoo ninayo. Ukimwomba akutumie picha, anakuambia niko mbali kidogo na sijapiga picha ukija utaiona mwenyewe lengo tu apate hiyo Sh. 10,000 yake. Utaambiwa nyumba iko karibu na barabara. Sasa ukienda utajuta kumfahamu, kiukweli inakera sana sana sana.

"Nadhani ifike wakati serikali iingilie kati, upangishaji wa nyumba pamoja na hili la madalali. Nyumba za kupangishwa ziwekwe kwenye mfumo rasmi ili kodi zisiwe za kukomoana. Kiukweli ukiongelea ugumu wa maisha suala la kodi za nyumba lazima ulitaje na wenye nyumba nao wanavimba vichwa mno."



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
IBILISI DIGITALI
WE USINTOE ROHO SIYAKIMBII MAPENZI BALI KUPANDA KWA GHARAMA ZAKE!
USIJITIE WAZIMU 'VITA HUIONI HUKO YUKRENI?
WEYE NKE' WA NTU!
WE MBONA MME WA 'NTU?
NIJE GETO HIYO VEEPE? ZEE ZIMA HUNA AIBU?
NIMEKUTESTI TU... NIMEFUNGA KWA REZMA NA PIA NNA SWAUMU.
WAACHE VITA! POMBE ZINAANGAMIA MABOMU YANAPASUA CHUPA ZA BIA HADI MIVINYO JAMANI. BAR ZINATEKETEA HIVI HIVI...
HANA AKILI ANAACHA KULILIA VIBINTI WAREMBO!
ETI' OOOH! KILA MWAKA ANA VIDONDA VYA TUMBO! KWANI VYENU?
SEMBE
KOBE
KILA KITU KINA-PANDA KASORO MSHAHARA!
UTAPANDAJE WAKATI NGAZI YAKE IPO KWA MWAJIRI NA IMEPOTEA?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...NENO LA MAMA LINAPONYA NJAA YA MTOTO

# Hali bado tete nchini Ukraine

## ■Russia yabadili kamanda wa vita
## ■Makombora yazidi kurindima

**KYIV,** UKRAINE

RUSSIA imeamua kubadilisha mbinu zake za kijeshi nchini Ukraine, baada ya kuwaondoa makamanda waliosimamia vita na kuwateua wengine wapya.

Ofisa mmoja wa magharibi amethibitisha kuwa Russia imepanga upya uongozi wa operesheni zake za kivita katika Ukraine, na kumteua Jenerali mpya mwenye uzoefu wa mapambono ya kivita nchini Syria ambaye sasa atasimamia vita hiyo.

Akizungumza na mwandishi wa BBC, Gordon Corera, kwa sharti la kutotajwa jina lake, chanzo cha taarifa hiyo kilisema kuwa kamanda wa wilaya ya kijeshi ya kusini mwa Russia, Jenerali Alexander Dvornikov, sasa ndiye anayeongoza uvamizi dhidi ya Ukraine.

"Kamanda huyo ana uzoefu mkubwa wa operesheni za Russia nchini Syria. Kwahiyo tunatarajia uongozi na udhibiti utaboreka ," kilisema chanzo hicho.

Uteuzi mpya ulifanyika katika jaribio la kuimarisha uratibu baina ya vikosi mbali mbali , kwani vikosi vya Russia vimekuwa vikipangwa na kuongozwa na wakuu tofauti.

Russia hadi sasa inahangaika kufikia malengo yake ya kivita, ikishindwa kuichukua miji muhimu kama vile Kyiv, kabla ya kuelekeza macho yake katika jimbo la Donbas mashariki.

Ofisa huyo alisema kuwa mbinu za Russia zimekuwa zikiwafanya warudishwe nyuma na vikosi vyenye askari wachache wa Ukraine wanaopigana kwa akili zaidi na kwa kushitukiza, licha ya Russia kufikiriwa kuwa na kikosi kikubwa chenye bataliani 100 zenye wanajeshi wenye ujuzi.

"Bila kubadili mbinu zake ni vigumu kwa Russia kufanikiwa kwa malengo yao waliyojiwekea wenyewe ," alisema ofisa huyo.

Watu watakiwa kuondoka Luhansk

Watu zaidi wanatakiwa kuondoka katika jimbo la Luhansk mashariki mwa Ukraine, huku mashambulizi ya makombora yakiendelea kuongezeka.

Wakati mashambulizi hayo yakiongezeka, idadi kubwa ya wanajeshi wamewasili katika jimbo hilo.

Gavana wa jimbo hilo, Serhiy Gaidai aliiambia televisheni ya kibinafsi kwamba asilimia 30 ya watu bado wamebakia katika miji na vijiji katika maeneo mbali mbali ya jimbo hilo.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, hali hiyo inakuja huku kukiwa na tahadhari kwamba Russia inapanga kuimarisha mashambulio yake katika jimbo la mashariki mwa Ukraine la Donbas , ambalo linajumuisha Luhansk, huku ikitaka kubuni ardhi inayoliunganisha na jimbo la Crimea ililolitwaa awali.

Zelensky atarajia jibu la kimataifa

Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, amesema anatarajia majibu madhubuti kutoka kwa jumuiya ya kimataifa baada ya kushambuliwa kituo cha treni na kuua zaidi ya watu 50.

Katika ujumbe wake wa kila siku wa video, Zelensky alisema wanatarajia hatua kali za kimataifa kwa uhalifu huo wa kivita. Alisisitiza wito wa vikwazo kamili vya nishati dhidi ya Russia na kutengwa kabisa kwa Benki za Urusi kimataifa.

Zelensky alisema usafirishaji wa nishati hutoa sehemu kubwa ya faida kwa Russia na hivyo uongozi wake unaamini kuwa ulimwengu utapuuza uhalifu wa kivita unaofanywa na jeshi lake.

Mamlaka za Ukraine zinasema watu 52 waliuawa na wengine 109 kujeruhiwa katika shambulio la roketi kwenye kituo cha treni katika mji wa mashariki wa Ukraine wa Kramatorsk, ambapo maelfu ya watu walikuwa wakisubiri kuhamishwa.

Ukraine ililaumu Russia kwa kuhusika na tukio hilo, jambo ambalo limepingwa.

Rais wa Halmashauri kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen, amempatia kiongozi wa Ukraine, Volodymyr Zelensky nyaraka za kuanza mchakato wa taifa hilo kujiunga na Umoja wa Ulaya.

Akimkabidhi nyaraka hizo, Von der Leyen alisema huo ndio mwanzo wa safari ya kujiunga na jumuiya hiyo.

Alisema wako tayari kuisaidia Ukraine kujaza maswali yaliyomo kwenye makaratasi hayo na kuongeza kuwa mchakato huo hautachukua miaka kama ilivyo kawaida na badala yake utachukua wiki kadhaa ili kukamilisha hatua hiyo. Von der Leyen alisema hayo kwenye mkutano wa pamoja wa waandishi wa habari kati yake na rais Zelensky mjini Kyiv alipokuwa ziarani pamoja na naibu wake Josep Borrel.

Kiongozi huyo ananuia kuwasilisha maombi ya Ukraine kwenye baraza la Ulaya katika kipindi cha majira ya joto ya mwaka huu.

Maofisa hao wa ngazi za juu katika Umoja wa Ulaya ni wa kwanza kwenda nchini Ukraine tangu Russia ilipolivamia taifa hilo.

Von der Leyen pia alizuru mji wa Bucha ambako mamia ya miili ya raia ilikutwa imezikwa baada ya vikosi vya Russia kuondoka kwenye mji huo.

Mwendesha mashitaka mkuu wa Ukraine Iryna Venediktova, alisema wanachunguza uwezekano wa uhalifu wa kivita nchini humo. Kutoka Bucha, ofisi ya mwendesha mashitaka mkuu imesema karibu watu 67 walizikwa katika kaburi la pamoja karibu na kanisa kwenye mji huo.

Iryna Venediktova alisema kwamba miili 18 imetambuliwa hadi sasa, 16 ikiwa na matundu ya risasi.

Alisema inamaanisha wanajeshi wa Russia waliwaua raia.

Ofisi yake inachunguza vifo hivyo na matukio mengine dhidi ya raia ili kuangazia iwapo yatakuwa ni uhalifu wa kivita. Umoja wa Ulaya pia unashiriki kwenye uchunguzi huo.

Ujerumani kuachana na nishati kutoka Russia

Nchini Ujerumani, taasisi ya utafiti wa kiuchumi, DIW imesema Ujerumani huenda ikaachana na utegemezi wa nishati inayoingizwa kutoka Russia wakati wa majira ya baridi ya mwaka huu.

Hatua hiyo itakuwa imefikiwa mapema kuliko matarajio ya awali ya serikali ya kuachana na utegemezi huo katikati ya mwaka 2024 ama baada ya hapo.

Suala la Ujerumani na Ulaya kuachana na utegemezi wa nishati kutoka nchi hiyo limechukua nafasi kubwa tangu vita hiyo ianze.

Nchini Slovakia, uamuzi wa serikali yake wa kupeleka mfumo wa kujilinda chapa S-300 nchini Ukraine, umewaghadhabisha wanasiasa wa upinzani wakisema hatua hiyo inaliweka hatarini taifa lao ingawa Marekani imesifu uamuzi huo.

Mfumo huo wa kujilinda na makombora uliundwa enzi ya Kisovieti.

Waziri mkuu wa zamani na mkuu wa chama cha Smer Robert Fico, alisema atatoa mwito wa kuitishwa kwa kikao maalumu cha kujadili kuiondoa serikali iliyoko madarakani, huku kiongozi wa chama cha Hlas Peter Pelegrini akiwatuhumu waziri mkuu Eduard Heger na waziri wa ulinzi Jaroslav Nad kwa kuwadanganya watu wa Slovakia kwa kueleza mfumo huo ulikuwa maalumu kwa kulinda mipango ya atomiki ya Slovakia na maeneo ya viwanda.



Mfanyakazi wa mji wa Kyiv, akiwa katika jengo lililoharibiwa na makombora ya Russia katika eneo la Borodyanka jana. **PICHA: REUTERS**

MAKALA

# TABIA HII HUZUIA MAENDELEO BINAFSI



Na Magabilo Masambu - 0689157789

**Asilimia 70 ya nishati yote Tanzania, hutumika kwa kupikia, ikifuatiwa na mafuta na umeme. Nishati kubwa inayoongoza kutumika kupikia ni tungamotaka (biomass).**

SIFA moja kubwa kwa sisi binadamu ni uwezo wa kufikiri tofauti miongoni mwetu. Maisha yetu yamekuwa mazuri na yenye kutegemeana kutokana na sifa hiyo.

Maana yake ni kwamba iwapo tutafikiri sawa, basi kuna hatari ya kutofanikiwa katika mambo mbalimbali.

Lakini kufikiri na kuwa na mitazamo tofauti, kusifanye tuwe vipofu katika kuyaona yale mazuri yanayofanywa na wenzetu waliofanikiwa katika nyanja mbalimbali, ili nasi tufanikiwe kama wao. Mafanikio huja kwa kujifunza kwa waliofanikiwa katika yale tunayoyahitaji sisi binafsi kuyafanya katika maisha yetu.

Ukitaka kuwa mvuvi mzuri mwenye mafanikio makubwa, huna budi kujifunza si tu kwa kila mvuvi bali kwa mvuvi aliyefanikiwa, vivyo hivyo katika maeneo mengine. Ukitaka kuwa mfanyabiashara mzuri basi inakubidi marafiki zako wengi wawe wafanyabiashara na si kila mfanyabiashara bali mwenye mafanikio katika aina ya biashara unayotaka kufanya.

Tabia moja mbaya kabisa katika maisha inayoweza kuzuia maendeleo yako ni kutokuona mema katika wanayofanya wengine. Si jambo baya kuwa na mtazamo tofauti katika yale wanayofanya wengine lakini utofauti huo ukusaidie katika kuboresha yale unayoyafanya wewe.

Aprili 2, mwaka huu, katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam, ulifanyika uzinduzi rasmi wa gari aina ya KP A72eV kwa jina lake likiitwa Keypee Motor ambalo ni la kwanza nchini Tanzania linalotumia nishati ya umeme, lililobuniwa na mchora katuni maarufu, Masoud Kipanya. Kwa maelezo yake mwenyewe, gari hilo litakuwa rafiki wa mazingira kwa sababu ya kutotumia mafuta.

Hili ni jambo jema sana kwa vijana wa Kitanzania kujifunza pamoja na kwamba tunajua kuwa nabii ni vigumu sana kukubalika kwao. Hatua hiyo inatakiwa kupongezwa sana na kila mwenye nia njema na mafanikio ya wengine. Lakini kinyume chake, ukifuatilia mazungumzo ya wengi hasa vijana ambao ndio wangelikuwa wa kwanza kujifunza ubunifu wa namna hiyo, wao ndio wa kwanza kubeza, kukosoa, kudhihaki na wengine kutukana.

Ni kweli kwamba ili jamii iendelee zaidi inahitaji watu wa sampuli hii lakini kwa upande wa pili, tabia hii inaweza kukufanya ukashindwa kuona na kujifunza mambo mazuri ya kimaendeleo katika kila jambo kwa mambo wanayofanya wengine. Nakubali kwamba ukosoaji huwa unamuimarisha yule anayekosolewa ikiwa atauchukulia kama ni ushauri kwake lakini unadumaza wakosoaji wenyewe kwa sababu watakuwa wameshajifungia mlango wa kujifunza ili wafanye zaidi ya anayekosolewa. Anayekosolewa atafanya maboresho kama atapima na kuona kama kuna upungufu katika jambo alilofanya.

Watu wengi wamekuwa na hofu ya kufanya mambo yao ya kimaendeleo kwa kuogopa kukosolewa, kubezwa au kutukanwa na watu wasioishi katika ndoto zao. Ni muhimu sana katika maisha kufanya jambo ambalo unalipenda hata likiwa haliwapendezi wengi ili mradi hujavunja sheria, taratibu na kanuni za nchi.

Ukiangalia wanaokosoa gari la Masoud hawakuwahi kutengeneza au kubuni chochote lakini ndio wanakuwa wa kwanza kusema hapa lingekuwa hivi na vile, mbele kungekuwa huko, lingekuwa refu kiasi hiki sasa mwambie hebu buni la kwako pia tuone hajui hata kulichora. Hapa ndipo tunapokwama katika kujiletea maendeleo binafsi.

Kwa mtazamo wangu, tuwape moyo wale wote wanaoonyesha mabadiliko katika jamii yetu. Tunachozidiwa na watu weupe ni tabia hii ya kudharau kila jambo na kujiona wajuaji kuliko wenye kazi zao. Tukibadilisha mtazamo huu tutawasaidia sana watu wengi wenye ubunifu na tutanufaika nao.

Natambua kuna wivu wa kibiashara. Leo Masoud kazindua gari lenye kutumia umeme, wanao uza mafuta lazima watavimba pengine kuleta fitina ili gari life kwa hofu kwamba hawatauza mafuta. Lakini tunachotakiwa kujua dunia hii ni pana sana, hivyo tuache kila mtu apate riziki kutokana na kipawa alichojaliwa na Mwenyezi Mungu. Mwenye mafuta atauza, anayetumia umeme atatumia na mwisho wa siku kila mmoja atanufaika na maisha yatasonga.

Kukazana kuua ndoto ya mtu hakutakusaidia kutimiza ndoto yako, ukiwa na nafasi ya kufanikisha mtu fulani kutimiza malengo yake, fanya kwa uwezo wako wote ili atimize ndoto yake maana maisha yana tabia ya kutegemeana. Leo unaweza kuwa umefanikiwa sana kesho ukaanguka na watakaokunyanyua ni wale uliowanyanyua wakati ulipokuwa umesimama.

Usijaribu hata kidogo kuwa sehemu ya kukwamisha mafanikio ya mwenzako iwe ni katika ushauri au aina yoyote ambayo matokeo yake litakuwa anguko lake ili mradi tu hayo mafaniko yake yasiwe na madhara kwa watu wengine kama kuharibu familia.

Mfano unampa mtu ushauri wa kupata mafanikio ili avunje ndoa yake na kujitegemea kwa kigezo kuwa sasa anayo mafanikio yatakayomfanya ajitegemee huo utakuwa si ushauri mzuri. Si kila ushauri ni wa kufanyia kazi, mwingine unausikiliza tu unaachana nao.

Mwisho, tuthamini kazi za wengine, tuwashauri kwa nia njema ya kufanya marekebisho na maboresho katika kazi zao ili ziwe nzuri zaidi. Tuwafanye wenye hofu ya kujaribu wajaribu. Huna haja ya kuogopa, jaribu kisha utarekebisha mbele ya safari. Kushindwa kujaribu ni kujaribu kushindwa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Kisa cha Kassim wa kustarehe, akafilisika



Na Adam Fungamwango

**"Ndugu Kassim ee, unawafanyaje sasa maisha ya watoto. Ulipokuwa huna kazi Kassim we, ulikuwa hutuki nyumbani. Sasa umepata kazi ndugu yangu ee, nyumbani huonekani.**

ORCHESTRA Mlimani Park iliundwa mwaka 1978 kutokana na asilimia 80 mpaka 90 ya wanamuziki waliokacha Dar International. Bendi hiyo pia ilimchukua mwimbaji tegemeo wa Juwata Jazz Band, Msondo Ngoma, Muhidini Mwalimu Gurumo kuongeza nguvu ya bendi hiyo.

Albamu, au rekodi za kwanza tu za bendi hiyo, ziliifanya kuwa tishio kwa bendi zingine zote nchini. Ukiachilia mbali wimbo wa 'Selina' uliotungwa na Joseph Mulenga ambao uliitambulisha bendi hiyo, wimbo wa 'Kassim' uliondokea kupendwa mno na mashabiki wengi, si wa Sikinde tu, bali hata wa bendi zingine. Kifupi ulipendwa na mashabiki wote wa muziki. Ulitungwa mwaka huo huo 1978 na Muhidini Gurumo.

Wimbo huo mbali na kuwa maarufu na kupendwa, ukazua misamiati mbalimbali kwa mashabiki wa muziki na hata ambao siyo, kwani kuna baadhi walikuwa wakitumia bila kujua imetokea wapi. Baada ya wimbo huo kupendwa sana, mwaka uliofuata, 1979, alitunga namba mbili ya wimbo huo. Ingawa wengi wanauita 'Kassim' namba mbili, wimbo huo jina lake halisi ni 'Kassim Amefilisika'.

Nyimbo hizo mbili zinamzungumzia mtu mmoja aitwaye Kassim, ambaye kabla hajapata kazi alikuwa akiishi vizuri na familia yake lakini baada ya kupata kazi, akawa haonekani nyumbani. Anashinda baa na vimada pamoja na rafiki zake akiwanunulia pombe, huku mke na watoto wakiteseka.

Baada ya miaka kadhaa kupita, nadhani alifukuzwa kazi kwani akafilisika na hata akienda baa hakuwa na mbwembwe kama zile za mwanzo. Hebu tuanze na Kassim namba moja.

*"Ndugu Kassim ee, unawafanyaje sasa maisha ya watoto. Ulipokuwa huna kazi Kassim we, ulikuwa hutoki nyumbani. Sasa umepata kazi ndugu yangu ee, nyumbani huonekani.*

*Unapokuwa huna pesa nyumbani hutoki, mwisho wa mwezi unapofika Kassim huonekani. Unapotoka kazini, unapitia kwenye baa, unapokuwa marafiki, ukiagiza, moja moto moja baridi. Ingine 'kipu chenji'. Lete sanduku moja. Unaporudi nyumbani umelewa kibao, unamwambia mama watoto, pesa zote zimeibiwa."*

Kutokana na wimbo huu, miaka ya 1980 na kuendelea kidogo, kukawa na misamiati kama vile mtu akilewa, anaitwa Kassim. Pia mtu anapotaka kwenda kupata kinywaji sehemu, basi atamwambia mwenzake, twende tukapate moja moto moja baridi. Na pia kama kuna mtu ambaye kwa wakati huo atakuwa na pesa na akazitumia kwa kunywa pombe na vimada, basi wenzake au jamii itakuwa ikisema kuwa "jamaa amekuwa Kassim wa kustarehe na kutumia."

Kusema kweli wimbo huu ulivuma kama moto wa nyika kwenye nyasi kavu wakati wa jua kali. Ndiyo maana wala haikushangaza, Gurumo na bendi yake ya Sikinde kutoa namba mbili yake, ambayo waliita 'Kassim Amefilisika' mwaka 1979.

Ni wakati ambao Sikinde ilikwenda kupeleka tena pigo lingine kwa Msondo, ikimchukua Hassan Rehani Bitchuka na Selemani Mwanyiro. Ndiyo maana kwenye wimbo wa Kassim namba moja kuna sauti ya waimbaji watatu tu, ambao ni Gurumo mwenyewe, Hamisi Juma, na Cosmas Chidumule.

Lakini kwenye Kassim namba mbili, kuna sauti ya Bitchuka, ambapo ameimba pamoja na waimbaji watatu walioimba namba moja. Wimbo huo una maneno yafuatayo:

"Ndugu mwenzenu, ninajiuliza, kwa mambo niliyoyafanya wakati ule ni mabaya sana. Nilikuwa napata pesa nyingi, lakini matumizi yangu, hali ya juu. Ninapokuwa na pesa mfukoni, nawatafuta marafiki tukatumie.

Sasa pesa zimemuishia, Kassim ee, hana la kufanya eee. Nikiingia kwenye baa ninaagiza chupa moja, lete chenji yangu haraka, na mie moja Kassim. Sina pesa ya mchezo.

Hapo zamani, nilikuwa naitwa Kassim wa kustarehe na wa kutumia, sasa sina pesa na marafiki zangu wote siwaoni hata mmoja kuja kunitembelea nyumbani kwangu, sijui nitafanyaje. Eee bwana Kassim ndiyo ukubwa huo, Kassim ee, hebu fanya shilingi moja hapo. Nakwambia niwaka ile ngumu."

Hayo ni mashairi ya wimbo wa 'Kassim Amefilisika', ambayo ilikuwa mwendelezo wa wimbo wa kwanza, ambao nao kama ule wa kwanza uliondokea kupendwa sana. Nao pia ukaleta misamiati mitaani. Ukimuomba mtu pesa kama hana, au hataki kukupa atasema 'nimewaka ile ngumu', msemo huu unatokana na wimbo huo.

Huyu ndiye Kasssim wa kustarehe na wa kutumia kama alivyoimbwa na Mlimani Park Orchestra, ambaye baadaye akafilisika.

Ni nyimbo ambazo zilizidi kumjenga Gurumo na kupewa uongozi wa bendi hiyo, kutoka na Abel Balthazar, lakini pia ukiifanya bendi hiyo kutoka kuwa bendi ndogo mpya, na kuwa bendi kubwa, ikishindana na Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma', zikawa bendi shindani au wakati wa jadi hadi leo hii.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Ajenda ya siri-25

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

USHAHIDI mwingine uliowasilishwa kortini hapo ni ule ambao Eddy aliupata Mbagala Charambe alipokwenda kwa hausiboi wa nyumba ya marehemu, Hussein.

Itakumbukwa alimkuta akicheza drafti na baada ya maongezi ya hapa na pale alimpa shilingi elfu hamsini na kufunguka kila kitu.

Hausiboi huyo aliyefanya kazi kwa miaka kumi, alisema anaamini ameondolewa kwa makusudi ili jambo fulani lifanyike na ameshuhudia mambo mengi pale ambayo hayapo, sawa na kubwa zaidi ni kwamba kuna siku aliwakuta Mtola na mama mwenye nyumba wamekumbatiana kimahaba bustanini.

"Nilishtuka sana na si siku hiyo tu, siku moja nilidhani mama hayupo, nikaingia ndani, nikawakuta Mtola na mama chumbani katika namna inayoonyesha kabisa ni mtu na mpenzi wake. Tangu siku hiyo mama alipatwa na wasiwasi mkubwa na akashinikiza mimi niachishwe kazi. Nikaachishwa, lakini baadaye mama akanifuata na kunipa pesa nyingi ili nisiseme chochote. Wale ni wapenzi na si mtu na mjomba wake kama alivyokuwa akidhani marehemu Chilambo," Hussein alimwambia Eddy wakati wa mahojiano.

"Mwanzoni tuliambiwa ni mtu na mjomba wake, alikuwa akija tu na kuondoka, baadaye sana alianza kuwa anakuja na kukaa hata siku tatu nne au wiki, anaondoka akikaa mwezi, akakuja tena, kila mtu akamzoea mle ndani, mpaka mimi nilipowabamba, lakini sidhani kama Tina na mzee Kalango na wote tuliokuwa tunaishi nao humo tulikuwa tunalitambua hilo, ila ni mimi tu nikaja gundua hilo, peke yangu, wakawa na hofu wakanitimua."

Ushahidi mwingine ni kwamba muda ambao bi Hellen aliingia ukumbini saa nne akiwa na Mtola ni kwamba alikuwa amepigiwa simu zaidi ya mara kumi na wafanyakazi wake, Tina, mzee Kalango na ndugu wengine wa marehemu na ndugu




**"Okay, nilisahau, Tinga kutana na shemeji yako, huyu anaitwa Mwahija." Alisema huku wote wakiwa wamemgeukia. Mwahija alitabasamu. Mwanya wake ulioonekana kwa usahihi zaidi ulizidi kumfanya apendeze zaidi.**

zake ambao walitaarifiwa tukio hilo, wakaungana pamoja kwenye Hospitali ya Mwananyamala kwa ajili ya mgonjwa hadi alipofariki dunia, lakini simu yake wakati huo wote ilikuwa imezimwa.

Inaonyesha kuwa nusu saa tu mke wa marehemu baada ya kuondoka nyumbani alizima simu yake na haijulikani alikokwenda hadi saa nne usiku ndipo alipoingia kwenye ukumbi wa Moonlight, Sinza.

"Kwa hali ya kwaida, mama anapoondoka nyumbani, hata kama hakuacha watoto ni lazima atapiga simu kuulizia usalama wa nyumba au ataacha simu wazi ili kama kuna tatizo apigiwe na watu aliowaacha. Haiwezekani simu izimwe kuanzia saa tisa mchana hadi saa nane usiku alipotoka ukumbini.

Tuna wasiwasi kuwa kuna kitu alikuwa anakifahamu kitatokea muda huo, hivyo hakutaka usumbufu kwani alikuwa kwenye starehe zake. Na pia inaonyesha kuwa mpangaji wa kitu hicho ni yeye mwenyewe au na washirika wake. Mume ameanza kuumwa saa 11:00 jioni na kufariki dunuia saa 2:00 usiku. Mke hakujua chochote hadi saa nane usiku alipowasha simu wakati anarejea nyumbani. Tuna wasiwasi na hilo." Ushahidi iliendelea kutolewa.

Utetezi ukadai kuwa baada ya kuonekana ukaribu au uhusiano usio wa kawaida kati ya Mtola, aliyepewa vidonge hivyo na Tina, inaonyesha kulikuwa na mawasiliano ya karibu kati yake ya mke wa marehemu, hivyo huenda alivichukua na kumpelekea bi Hellen bila kuonekana na yoyote, ambaye alitekeleza jukumu la kumuua mumewe, kwani urejeaji wake nyumbani wa kisirisiri kama shahidi mzee Kalango alivyodai, unatia shaka.

Hapo ndipo upande wa utetezi alipomaliza rasmi kutoa utetezi wake.

Jaji Msemwa alisimama na kusema wameusikiliza upande wa utetezi na kilichobaki ni kwenda kufanya majumuisho na kutoa hukumu.

"Tutatoa hukumu wiki ijayo." Alimaliza na watu wote wakasimama kupisha majaji watatu kuondoka.

************************

Eddy wakati akitoka na mpenzi wake Mwahija, alikutana na wakili Tinga nje ya mahakama. Wakakumbatiana kana kwamba ndiyo kwanza wanaonana.

"Nadhani kazi imekwenda vizuri." Eddy alimwambia mwenzake.

"Siyo mbaya, ila tusubiri hukumu wiki ijayo, nadhani kazi umeifanya vizuri tu." Tinga alijibu.

"Okay, nilisahau, Tinga kutana na shemeji yako, huyu anaitwa Mwahija." Alisema huku wote wakiwa wamemgeukia. Mwahija alitabasamu. Mwanya wake ulioonekana kwa usahihi zaidi ulizidi kumfanya apendeze zaidi.

"Habari yako shemeji."

"Nzuri tu, za kwako."

"Salama, karibu sana."

"Yaani unakaribisha shemeji yako mahakamni." Eddy alidakia, halafu wote wakaangua vicheko.

"Shemeji, huyu mtu wako, ndivyo alivyo hivi."

"Mi mwenyewe nishamzoea siku hizi, wala hanipi taabu." Mwahija alijibu na vicheko vikazidi.

Ghafla watu wawili walisimama mbele yao. Ni bi Mtupeni na mumewe. Walisimama, lakini bila kuingilia mazungumzo.

Eddy alijua ni yeye anahitajika. "Samahani, naomba niwasikiilize kidogo hawa wazee wangu." Hakusibiri yeyote aseme lolote, alivuta hatua chache na kwenda nao pembeni.

"Baba tunashukuru sana, naona kama kesi inakwenda vizuri hivi." Bi Mtupeni alimpa pongezi.

"Ahsateni sana mama pamoja na baba, lakini mimi nadhani tusubiri wiki ijayo hukumu itoke, ndipo tutapongezana, hapa bado kidogo."

"Sijui ninacheza ngoma gani mimi kama Tina atashinda kesi hii."

"Ni kiasi cha kusubiri tu." Eddy alijibu na kutoa kiasi cha elfu ishirini, kila mmoja akampa shilingi elfu kumi.

"Wazee wangu, hizi ni za nauli."

"Nashukuru mwanangu, Mungu akubariki, akuongezee zaidi na zaidi. Kila utakachokishika kiwe na neema." Dua hizo zilitoka kwa bi Mtupeni ambaye yeye ndiye mwongeaji zaidi kuliko mumewe.

Huyu ndiye mama mlezi wa Tina Kauzeni, anayetuhumiwa kumuua bosi wake Chilambo.

Haikuishia hapo. Eddy alidakwa na watu viongozi wa mashirika yasiyo ya kiserikali, yanayodili na unyanyasaji wa kijinsia na hasa wasichana wadogo. Mengine yalikuwa ya kuwasaidia wasichana wanaofanya kazi za ndani ambao walionekana kuguswa na kesi hiyo.

Eddy alionekana kushangaa, kwa sababu yeye hakuwa wakili kwenye kesi hiyo na wala hakusimama mahakamani. Alichofanya ni kupeleleza na kuhakuna mtu aliyemuwna. Alifanya kazi peke yake hadi alipokamilisha na kumkabidhi Tinga.

Alimwita Tinga. "Hebu wajibu maswali yao, mimi sihusiki na maswali haya." Alijitoa.

Ni kama vile tayari walishajua mtu aliyekusanya upelelezi wote mgumu uliokuwa umejifungafunga na kuuweka wazi ni yeye.

ITAENDELEA JUMAPILI

# MADAM FLORA

## AWAGEUKIA WATU WASIOJIWEZA



MIONGONI mwa waimbaji wa Injili wenye mafanikio hapa nchini ni Madam Flora, ambaye kupitia nyimbo zake ameweza kupata wafuasi wengi.

Kupitia nyimbo zake amegusa mioyo ya watu kiasi ambacho imekuwa vigumu kuondoa hisia zake kwa watu mbalimbali wanao msikiliza.

Katika mahojiano maalum aliyoyafanya na Gazeti hili, Madam Flora anasema kwa sasa anataka kufika mbali kwa kusaidia zaidi wasiojiweza kupitia taasisi yake ya Faraja Initiatives.

"Nataka kuwa na watu karibu katika kupambana na Ukimwi na Malaria, pia kutoa msaada wa kimaadili, maarifa na kiuchumi kwa wanawake, watoto yatima na makundi mengine yaliyopo kwenye mazingira magumu," anasema.

Anaongeza "Dira kubwa ya shirika hili ni kuhakikisha kuimarishwa kwa maisha na usawa kwa wanawake, watoto, yatima, wazee na makundi yaliyotengwa na jamii Tanzania na hilo tumeanza kulifanikisha."

Madam Flora amesema ndani ya mwaka huu tayari shirika hilo limewafikia watu wengi.

## CUTSLEEVE RIDDIM' KUSIMAMISHA DUNIA

LEBO ya Cutsleeve Recordsn, inatarajia kuzindua albamu yake mpya inayoitwa 'Cutsleeve Riddim'yenye mkusanyiko wa nyimbo kutoka kwa wasanii kutoka mataifa tofauti.

Jdart ambaye ndio bosi wa Lebo hiyo iliyopo nchini Japan, amesema lengo la kutoa albam hiyo ni kubadilisha ulimwengu wa muziki, hivyo anaamini mashabiki wa mataifa mbalimbali watafurahia kazi hiyo mpya.

Wasanii kutoka Tanzania ni Madematrix, Lody Music, Melodyne, wengine kutoka mataifa mengine ni Teejay, Chronic Law, Shatti, Int3ll, Jahvillani, Onsoundmynd, Cashan, Iquu, Zebee, Jah Sam, Slyngaz, B.J Goldman, Iamstylez Music, Galiano na wengine.



# Top Boy kusaka kolabo Bongo

Msanii wa kizazi kipya kutoka nchini Uganda, David Kalupa a.k.a Top Boy, ametua Tanzania kufanya kolabo na wasanii mbalimbali.

Akizungumza na Nipashe, Top Boy amesema huo ni mwendelezo wa kufanya soko la muziki wake Afrika Mashariki kwani anaamini ana mashabiki wengi sana nje ya Uganda.

" Nimekuja hapa Tanzania kufanya kolabo na wasanii mbalimbali, baada ya kufanya kazi na Awilo Longomba sasa nimefanya kolabo na Christian Bella. Pia nipo kwenye mazungumzo na Harmonize hii yote ni mapenzi yangu kwa Tanzania maana wamekuwa wakinipa sapoti kubwa," amesema Top Boy.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# PSG KUMBAKIZA MBAPPE

Wapo tayari kumpa pauni milioni 150 ili kuongeza mkataba na...

**PARIS, UFARANSA**

PARIS ya Paris St-Germain ipo tayari kumpa mshambuliaji Kylian Mbappe ada ya usajili ya pauni milioni 150 ili kumbakisha katika klabu hiyo kwa misimu mingine miwili, kwa mujibu wa mchambuzi wa soka wa Hispania, Guillem Balague.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 unamalizika msimu huu wa joto na aliripotiwa kuwa amefikia makubaliano binafsi na Real Madrid miezi kadhaa iliyopita.

Lakini PSG wanatamani kumbakisha na pia watatoa mshahara wa jumla wa pauni milioni 21 kwa mwaka.

Licha ya pendekezo hilo la faida kubwa, Madrid inasalia kuwa mahali anapopendelea zaidi.

Akizungumza baada ya kufunga mabao mawili katika ushindi wa Jumapili wa Ligue 1 dhidi ya Lorient, Mbappe aliambia vyombo vya habari: "Sijafanya uamuzi wangu, kuna mambo mapya ya kuzingatia. Vipengele gani? Vipengele vipya tu."

Balague amesema "vipengele hivyo vipya" ni hamu ya mshambuliaji huyo kufanya mazungumzo na klabu hiyo ya Hispania baada ya ofa mpya ya kifedha iliyo wazi kwake.

PSG inayomilikiwa na tajiri kutoka nchini Qatar inaweka shinikizo kwa mshambuliaji huyo wa Ufaransa kujitolea kusaini mkataba mpya na kusalia hadi baada ya Kombe la Dunia nchini Novemba na Desemba.

Tayari walikuwa wamempa ada ya kumsajili ya pauni milioni 125 lakini sasa wako tayari kuongeza hiyo kwa pauni milioni 25.

Mbappe anawakilishwa na wazazi wake, ambao hawakubaliani juu ya hatua yake inayofuata, lakini mwishowe uamuzi utakuwa wa mchezaji.

Ikiwa atasalia, washauri wake watapokea pauni milioni 42 kama malipo ya kamisheni kutoka kwa PSG.

Real Madrid wametulia kuhusu hali hiyo kwa vile wanajua kuwa wana makubaliano na wamepunguza nia yao ya kumnunua Erling Braut Haaland, hiyo ni imani yao katika kukamilisha dili la kumnunua Mbappe.

## KWA UFUPI

### SALAH AKATAA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Misri Mohamed Salah amesema sio wakati muafaka kwake kuzungumzia mazungumzo yake ya mkataba mpya yanayoendelea na klabu hiyo, ambayo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ameitaja kuwa "hali nyeti". ***(Sky Sports)***

### DEMBELE KUTUA PSG

BARCELONA wanaamini winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, ambaye atakuwa mchezaji huru msimu wa joto, atajiunga na Paris St-Germain ikiwa mshambuliaji Kylian Mbappe mwenye miaka 23, ataondoka katika klabu hiyo ya Ufaransa. ***(El Nacional)***

### HALAAND NA MAN

MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, anahofia Manchester United haitaweza kufikia matarajio yake uwanjani anapofikiria kuhama kwake. ***(ESPN)***

### BOWEN ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle ina nia ya kumsajili mshambuliaji wa West Ham, Jarrod Bowen mwenye umri wa miaka 25. ***(90min).***

### BELLINGHAM AWANIWA

MANCHESTER City na Real Madrid zote zinavutiwa na kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 18. ***(Fichajes)***

### NUNEZ KUTUA EPL

MSHAMBULIAJI wa Benfica, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 22, amethibitisha kuwa anabadilisha mawakala kabla ya dirisha la usajili la majira ya joto, huku timu za Ligi Kuu England, Arsenal na Manchester United zikitajwa kumuwania mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay. ***(Metro)***

### PEPE KUUZWA

ARSENAL wako tayari kumuuza winga wa Ivory Coast, Nicolas Pepe mwenye umri wa miaka 26, kwa euro milioni 30 msimu huu wa joto. ***(Calciomercato)***

### HAZARD ATAJWA ARSENAL

ARSENAL wamefanya mikutano na Real Madrid kuhusu uwezekano wa kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31. ***(Foot Mercato).***

### PHILLIPS ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle ipo tayari kumsajili kiungo wa Leeds United, Kalvin Phillips. Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 26 pia amekuwa akihusishwa na Manchester United. ***(Mail)***

### MADUEKE AWANIWA

KLABU ya Aston Villa inamfuatilia winga wa PSV, Noni Madueke mwenye umri wa miaka 20. Leicester City pia wanavutiwa. ***(Sport)***

### OZIL KUTUA MAREKANI

KIUNGO wa kati wa Fenerbahce na Ujerumani, Mesut Ozil mwenye umri wa miaka 33 anaweza kujiunga na klabu ya Ligi Kuu ya Marekani, MLS, Inter Miami. ***(Metro)***


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MACHESTER CITY
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.11
X | 3.49
2 | 3.24

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GERRARD: KANE ATAPATA FURAHA KUBAKI SPURS



**LONDON, England**

STEVEN Gerrard amesema Harry Kane hahitaji kujiunga na timu nyingine ili kupata furaha, kwani itakuwa na maana zaidi kushinda kombe akiwa na Tottenham kuliko klabu nyingine yoyote.

Kane alibaki Tottenham kwa ajili ya msimu wa 2021-22, licha ya kuomba kuondoka kaskazini mwa London baada ya Manchester City kuwasilisha ombi la zaidi ya pauni milioni 100.

Baada ya kuanza vibaya msimu nahodha huyo wa timu ya taifa ya England amerejelea kiwango cha juu tangu katikati ya Desemba.

Tangu Desemba 19, Kane amefunga mabao 14 na kusaidia matano zaidi katika mashindano yote.

Katika muda huo, ni Kylian Mbappe (20) na Karim Benzema (24) pekee ambao wamehusika moja kwa moja kwenye mabao zaidi ya 19 kati ya wachezaji kutoka ligi tano bora za Ulaya.

Licha ya kiwango cha kuvutia cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 katika kipindi cha pili cha msimu, Tottenham itamaliza msimu bila taji lolote huku Kane akingoja kombe.

Lakini Gerrard, ambaye alitumia msimu mzima isipokuwa mmoja wa uchezaji wake wa miaka 18 akiwa na Liverpool ya utotoni, anatumaini kuona mtani wake akisalia Tottenham kwa muda mrefu zaidi.

"Ninavutiwa na uaminifu wake kwa Tottenham na bila shaka, nina uhakika amekuwa akimjaribu mara nyingi kupata kombe," alisema Gerrard.

"Mashabiki wa Spurs wanapaswa kumfurahia na kustaajabia uaminifu ambao amewapa. Unaweza kuona mtu ambaye anatamani sana mafanikio akiwa na Tottenham na ninavutiwa sana na hilo."

# Salah akataa kuzungumzia mkataba

**LIVERPOOL, England**

MOHAMED Salah amebainisha hataki kuzungumzia kuhusu kukwama kusaini mkataba mpya na Liverpool kwa sasa, kwa sababu ya umuhimu wa mbio za wekundu hao kwenye taji la Ligi Kuu England.

Kikosi hicho cha Jurgen Klopp kinapambana na kuwania ubingwa wa Ligi Kuu wakati watakapoivaa Manchester City leo Jumapili wakiwa wamepitwa pointi moja katika msimamo.

Halafu watacheza na Benfica kwenye mchezo wa pili war obo fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya Jumatano kabla kucheza na City pale Wembley kwenye kombe la FA.

Mazungumzo ya Salah kuhusu mkataba - ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu 2022/23 - amekuwa muhimu sana kwa kikosi hicho cha wekundu hao msimu huu, na akizungumzia kuelekea mchezo huo wa leo pale Etihad, raia huyo wa Misri aliulizwa kuhusu mkataba mpya kama atasaini hapo Anfield.

"Siwezi kusema ndio, siwezi kusema hapana. Nimezungumza mara milioni hapo kabla kuhusu nini ninachotaka, lakini siwezi kwenda kwa undani -siwezi kuzungumzia kuhusu mkataba mpya kwa sasa, kwa sababu timu inahitaji ushindi," alisema Salah.

"Sina cha kuzungumza, kiukweli nizungumze nini? Kuna vitu vingi watu hawavijui. Siwezi kuwa mbinafsi. Tupo kwenye wakati muhimu zaidi kwa timu sasa.

"Hivyo nataka kuzungumza kuhusu timu, kuangalia kile kilichopo mbele yetu. Nina matumaini tutakwenda mbali zaidi na tutaangalia nini kitatokea kuhusu mkataba mpya.



CHEZA USHINDE KASINO
JISAJILI CHEZA SHINDA

# DSTV YAZIDI KUNOGESHA BURUDANI

**Na Dennis Fussi**

WATEJA wa DStv wanaingia robo ya pili ya mwaka huu mabega juu kwani wamehakikishiwa nyongeza ya burudani katika vifurushi vyao na ofa kabambe kwa wateja wapya wanaojiunga.

Hayo yamebainishwa na Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo wakati alipokuwa akizindua kampeni maalum ya DStv ambayo inaambatana na ofa kwa wateja wapya na kuongezwa kwa muda wa baadhi ya vipindi pendwa ikiwemo tamthilia maarufu ya Jua Kali.

Alisema tamthilia kongwe ya Huba imeingia msimu mpya wa 11 ambao ni moto wa kuotea mbali ambapo waigizaji mahiri kama Kibibi, Devi, Tesa, Tima, Roy, Kashauro na wengineo wamejipanga kikamilifu kuwapa watazamaji burudani ya karne katika msumu huu.

"Patashika ipo kwenye msimu mpya wa tano wa tamthilia namba moja ya Jua Kali, ulioanza mwezi huu ambapo ili kukata kabisa kiu ya mashabiki wake, sasa inaonekana kwa siku tano za wiki kuanzia Jumatano hadi Jumapili," alisema Shelukindo.

"Tamthilia iliyozua gumzo mitaani ya Pazia nayo imerejea tena kwa nguvu mpya kwa msimu wake wa nne na inaonyeshwa mara tatu kwa wiki kuanzia Jumatatu hadi Jumatano saa moja na nusu jioni.

"Huku nako kimeumana kwani Regina amejifungua mtoto wao na Edu. Juma Mdoe sasa anaishi na Eliza, Regina ameenda kuishi na Miriam huku Gloria akiamua kukimbilia kijijini; Huwezi kuamini! Sasa Henry ni mfanyakazi katika duka la vifaa vya ujenzi la Eliza ambalo awali alikuwa analimiliki. Ni nini kimetokea hadi mambo yakabadilika kiasi hiki? Bila shaka hutakubali kupitwa na utamu na msisimko wa tamthilia hii maridhawa ya Pazia."

Kwa wale wapenzi wa kandada, Ligi kuu ya England imefika mahali patamu kwani sasa ni kuelekea hatua za mwisho huku vigogo wakipigana vikumbo kuutwaa ubingwa na vibonde wakikabana koo kujinusuru na kushuka daraja.

Mchakato wa kuelekea Kombe la dunia nao umeshika kasi na DStv inakuletea matukio mbalimbali ya mandalizi ya michuano hiyo ikiwemo mechi za kufuzu kwa kombe la dunia.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha kuwa wateja wetu wanaendelea kupata burudani isiyo na kikomo huku pia tukiwapa ofa wateja wetu wapya ili waweze kujiunga na DStv wasipitwe na burudani hizi" amesema Shelukindo.

Amesema kwa wale ambao bado hawajajiunga na DStv, sasa wanaweza kujiunga kwa bei ya punguzo ya Sh. 59,000 tu ambapo watapata seti pamoja na kifurushi cha DStv Poa cha mwezi mmoja.

Amewataka wale ambao hawajajiunga na DStv kuchangamkia ofa hii maalum kwani itakuwepo kwa muda wa miezi mitatu tu. Pia amewahakikishia wateja wa DStv kuwa burudani inazidi kuongezwa katika vifurushi vyao hivyo waendelee kulipia vifurushi vyao kulingana na mahitaji yao.



Mtayarishaji wa filamu nchini, Samwel Isike akizungumza machache akiwa na waigizaji wa tamthilia ya Pazia, Jacqueline Wolper na Nasma Hassan, inayoruka ndani ya DStv chaneli ya Maisha Magic Bongo namba 160 katika uzinduzi wa kampeni mpya ya DStv iitwayo Ewaaa! iliyofanyika jana jijini Dar es Salaam katika makao makuu ya ofisi za MultiChoice Tanzania zilizopo Kinondoni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Coastal vs Kagera FA kesho

**Na Cheji Bakari, Tanga**

UONGOZI wa Coastal Union umebainisha kuwa umejifunza kutokana na makosa yaliyofanywa na mabeki wake katika mechi dhidi ya Simba, lakini sasa wanajiandaa kuikabili vilivyo Kagera Sugar katika mchezo wa kombe la Shirikisho (FA) katika uwanja wa Mkwakwani kesho Jumatatu.

Baada ya kufungwa na Simba, Coastal imebakiwa na pointi 21 baada ya kucheza michezo 19 ikishushwa nafasi moja chini kutoka ya 11 hadi 12 kwenye Ligi Kuu.

Msemaji wa Coastal, Miraji Wandi amesema uzembe wa mabeki ndio uliochangia wapo kufanya vibaya, lakini kwa sasa wamejipanga.

"Uzembe wa mabeki wetu ndio umetugharimu katika ile mechi ya Simba, lakini mwalimuameyaona hayo na amejipanga vizuri kuivaa Kagera Sugar," alisema Wandi.

"Timu ipo kwenye mazoezi makali na inajifua kuhakikisha inaibuka na ushindi kwenye mchezo huo."

SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI


"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 10/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:15 | 4316 | Heerenveen vs Groningen | 2.36 | 3.18 | 2.93 |
| 13:30 | 1441 | Yeni Malatyaspor vs Giresunspor | 3.29 | 3.29 | 2.14 |
| 13:30 | 5699 | Genoa vs Lazio | 3.99 | 3.49 | 1.88 |
| 14:00 | 1094 | Bordeaux vs Metz | 1.93 | 3.41 | 3.96 |
| 14:00 | 3006 | St Mirren vs Rangers | 9.13 | 4.96 | 1.31 |
| 14:00 | 5001 | Ufa vs Sochi | 2.88 | 3.03 | 2.48 |
| 14:30 | 1242 | Sandhausen vs Dynamo Dresden | 2.29 | 3.16 | 3.06 |
| 14:30 | 3985 | Paderborn vs Karlsruher SC | 2.12 | 3.52 | 3.08 |
| 15:00 | 5771 | Osasuna vs Alaves | 1.93 | 3.32 | 4.13 |
| 15:30 | 1929 | PSV Eindhoven vs Waalwick | 1.11 | 8.33 | 16.85 |
| 15:30 | 2282 | Vitesse Arnhem vs Cambuur | 1.51 | 4.34 | 5.33 |
| 16:00 | 1445 | Sassuolo vs Atalanta | 3.25 | 3.65 | 2.05 |
| 16:00 | 2802 | Adana Demirspor vs Altay | 1.63 | 3.84 | 4.99 |
| 16:00 | 2814 | Leicester vs Crystal Palace | 2.32 | 3.35 | 2.95 |
| 16:00 | 3036 | Angers vs Lille | 3.27 | 3.12 | 2.28 |
| 16:00 | 3257 | Sivasspor vs Basaksehir | 2.69 | 3.24 | 2.54 |
| 16:00 | 3503 | Napoli vs Fiorentina | 1.73 | 3.76 | 4.41 |
| 16:00 | 4904 | Venezia vs Udinese | 3.35 | 3.25 | 2.15 |
| 16:00 | 5422 | Norwich City vs Burnley | 2.84 | 3.09 | 2.54 |
| 16:00 | 5544 | Brest vs Nantes | 2.57 | 3.12 | 2.82 |
| 16:00 | 5641 | Brentford vs West Ham | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 16:00 | 5852 | Monaco vs Troyes | 1.35 | 4.93 | 8.26 |
| 16:30 | 3682 | VfL Bochum vs Bayer Leverkusen | 3.91 | 3.91 | 1.79 |
| 16:30 | 3862 | Spartak Moscow vs Arsenal Tula | 1.45 | 4.27 | 6.36 |
| 16:30 | 4010 | Crotone vs Ternana | 2.43 | 3.12 | 2.87 |
| 16:30 | 4305 | Cosenza vs Monza | 4.75 | 3.42 | 1.73 |
| 16:30 | 5285 | Ascoli vs Reggina | 2.06 | 3.12 | 3.66 |
| 17:00 | 1023 | Fulham vs Coventry | 1.47 | 4.36 | 5.94 |
| 17:15 | 4494 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.73 | 3.13 | 2.68 |
| 17:30 | 1463 | Portimonense vs Famalicao | 2.90 | 3.10 | 2.46 |
| 17:30 | 1568 | St. Gallen vs FC Basel | 2.29 | 3.49 | 2.84 |
| 17:30 | 2481 | FC Lugano vs FC Sion | 1.83 | 3.44 | 4.19 |
| 17:30 | 4525 | Santa Clara vs GD Estoril | 2.24 | 3.09 | 3.28 |
| 17:45 | 4694 | Heracles Almelo vs Feyenoord | 5.13 | 4.24 | 1.54 |
| 18:05 | 4373 | Lens vs Nice | 2.30 | 3.31 | 3.06 |
| 18:30 | 4447 | Manchester City vs Liverpool | 2.11 | 3.49 | 3.24 |
| 19:00 | 1272 | Perugia vs Pisa | 2.63 | 2.93 | 2.78 |
| 19:00 | 4602 | Roma vs Salernitana | 1.26 | 5.61 | 10.02 |
| 19:30 | 2464 | Rostov vs Lokomotiv Moscow | 2.40 | 3.06 | 2.97 |
| 19:30 | 3597 | Elche vs Real Sociedad | 3.79 | 3.34 | 2.01 |
| 20:00 | 2096 | Strasbourg vs Lyon | 2.45 | 3.32 | 2.82 |
| 20:00 | 4738 | Vitoria Guimaraes vs Porto | 6.17 | 4.18 | 1.48 |
| 20:05 | 4214 | Cukaricki St vs Partizan | 6.03 | 4.09 | 1.45 |
| 20:30 | 3976 | RB Leipzig vs Hoffenheim | 1.50 | 4.60 | 5.40 |
| 20:30 | 4430 | Fenerbahce vs Galatasaray | 1.92 | 3.58 | 3.63 |
| 20:30 | 5927 | Bursaspor vs Kocaelispor | 1.92 | 3.36 | 3.56 |
| 21:00 | 3481 | PEC Zwolle vs AZ Alkmaar | 4.57 | 3.63 | 1.71 |
| 21:45 | 3219 | Torino vs AC Milan | 4.01 | 3.46 | 1.88 |
| 22:00 | 1136 | Marseille vs Montpellier | 1.53 | 4.24 | 5.65 |
| 22:00 | 3762 | Levante vs Barcelona | 5.71 | 4.66 | 1.49 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Aprili 10, 2022
Nipashe



## PSG kumbakiza Mbappe

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba (kutoka kushoto) Erasto Nyoni, Peter Banda na Meddie Kagere wakifanya mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Polisi Tanzania utakaopigwa leo kwenye uwanja wa Ushirika Moshi, Kilimanjaro. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA, POLISI KAZI IPO LEO

Ni katika mchezo wa Ligi Kuu ikipambana kuifukuzia Yanga, huku ikitoka kuifumua Coastal Union...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga Alhamisi iliyopita, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, leo watakuwa kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi, mkoani Kilimanjaro kucheza dhidi ya wenyeji Polisi Tanzania.

Ni mechi ya kukamilisha raundi ya 19, kwani ni timu hizo mbili tu ndiyo hazijacheza mechi hiyo, ambayo awali iliahirishwa kutokana na Simba kuwa kwenye kinyang'anyiro cha mechi za kimataifa.

Simba itaingia uwanjani leo, ikihitaji ushindi ili kuendelea kuwa na ndoto ya kuutaka tena ubingwa kwa mara ya tano mfululizo.

Sare na kupoteza ni kuendelea kuwapalilia njia watani zao wa jadi Yanga kuelekea kwenye ubingwa wao wa kwanza baada ya misimu minne.

Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco amesema kuwa mechi itakuwa ngumu kwa sababu mbalimbali, lakini wamejipanga vema kushinda kwa ajili ya wanachama na mashabiki wa Simba.

"Tumecheza mechi ngumu dhidi ya Coastal Union, tumesafiri masaa sita baada ya kucheza mechi hiyo ngumu na kesho (leo) tunakwenda kucheza mechi nyingine ngumu kwenye uwanja mbaya," alisema Pablo.

"Hatujatapata fursa ya kuweka miili sawa wala kufanya mazoezi. Lakini tunakwenda kupambana. Tutakwenda kucheza kwa ajili ya wanachama na mashabiki wa Simba, pamoja na wapenzi wa soka. Tutajitahidi kubadilisha mfumo kwa sababu Polisi Tanzania ni timu nzuri, inayocheza vizuri pia.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo amesema wanakwenda kucheza na timu bora ya Simba ambayo huwasumbua kila wanapocheza nayo, lakini wamejiandaa kupambana kupata pointi tatu kwa ajili ya kufukuzia moja ya nafasi tatu za juu ambazo zitawapa fursa kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao kutokana na kwamba zitakwenda timu nne.

"Ni timu inayotusumbua sana, lakini kwa sasa tunaangalia namna ambavyo tumejiandaa. Tunakwenda kupambania pointi tatu.

"Naamini Polisi Tanzania ni timu bora sana, hasa ikicheza nyumbani, timu haina majeruhi, ni namna tu ambavyo tutachagua kikosi cha wachezaji 11 wanaokuwakilisha, tunataka kushinda ili tutimize ndoto yetu ya kumaliza kwenye nafasi tatu za juu," alisema Mketo, kiungo wa zamani wa Simba.

Wakati Simba ikikamata nafasi ya pili kwa pointi 40, Polisi Tanzania iko kwenye nafasi ya tisa ikiwa na pointi 23.

## Ni Yanga vs Geita FA leo

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Yanga kinashuka dimbani leo kukabiliana na Geita Gold FC kwenye mchezo wa robo fainali ya kombe la Shirikisho (FA), utakaopigwa katika uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Yanga imetinga hatua ya robo fainali baada ya kuifunga Biashara United na kudhamiria kufanya kweli msimu huu ikiwemo kucheza fainali ya kombe la shirikisho.

Kikosi cha Yanga kinachonolewa na Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi kimejipanga kinaondoka na ushindi kwenye mchezo huo, baada ya kutoka kuifunga Azam FC mabao 2-0 kwenye Ligi Kuu.

Katika mchezo huo Nabi amewapa majukumu mapya nyota wake kuhakikisha wanaendelea kupata matokeo mazuri katika mchezo huo ili kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa FA msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema wachezaji wote wana viwango vizuri lakini kila mmoja anahitaji kuwajibika kulingana na timu watakayokwenda kucheza nao.

Alisema mchezo huo utakuwa wa ushindani mkubwa na kuhakikisha wanapambana kutafuta ushindi katika mchezo huo ili kufikia malengo ya kuhakikisha wanacheza nusu fainali.

"Mechi itakuwa ya ushindani mkubwa, maandalizi yanaendelea vizuri na kikosi kipo tayari kwa ajili ya kucheza mchezo dhidi ya Geita Gold na kuhakikisha tunapata matokeo mazuri na kucheza nusu fainali," alisema Nabi.

Alisema wanaingia kwa kuwaheshimu Geita Gold kwa sababu hakuna timu iliyo rahisi ambayo imeingia kucheza hatua ya robo fainali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >